**Watu** 15 wafariki kwa corona Zanzibar, wengine 390 waugua

UKURASA 2



**Mawakili** utetezi kesi ya Ole Sabaya wagonga mwamba

UKURASA 3



**PSG bado wampigia hesabu Pogba**

UKURASA 20


# Nipashe

Alhamisi Agosti 12, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580670

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# NMB yazindua mikopo urasmishaji wa makazi

UKURASA 16

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**AU KUIPA TANZANIA DOZI MILIONI 17 CHANJO CORONA**

UMOJA wa Afrika umeitengea Tanzania dozi milioni 17 za chanjo za...

UKURASA WA 3

**MUSIBA AAMRIWA KUMLIPA FATMA KARUME BIL. 7.5/-**

MAHAKAMA Kuu Zanzibar imemwamuru Cyprian Musiba na Gazeti...

UKURASA WA 4

**KORTI: VIGOGO NIDA WANA KESI YA KUJIBU**

ALIYEKUWA Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa...





Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi (wapili kushoto), akizindua mpango wa kitaifa wa urasimishaji makazi, katika Kijiji cha Igawa, Kata ya Igawa, wilayani Mbarali, mkoani Mbeya jana. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), Kaimu Ofisa Mkuu Mkaguzi wa ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Mary Makondo, na Mkufunzi wa Chuo cha Ardhi, Dk. Victoria Mwakalinga. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Vigogo Bandari mikononi mwa PAC



UKURASA 2



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Shaka Hamdu Shaka. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Gazeti la Uhuru lajifungia kisa upotoshaji kuhusu Rais

• **Serikali** yashusha rungu, mkurugenzi, wahariri waandamizi wasimamishwa kazi... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **GOMES AANZA MKWARA SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Vigogo wa Bandari mikononi mwa Bunge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) Jumatatu ijayo inatarajia kuanza kuwahoji watendaji wa taasisi na mashirika ya umma kuhusu hoja mbalimbali za ukaguzi zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/20.

Kwa mujibu wa uongozi wa kamati hiyo nyeti, Mamlaka ya Bandari (TPA) itakuwa ya kwanza kuhojiwa.

Akizungumza jana na Nipashe jijini Dodoma jana, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, alisema:

"Leo (jana) Waziri wa Fedha anakuja kwenye kamati kuwasilisha 'draft' ya muswada, mahojiano ya mashirika na serikali yataanza Jumatatu wiki ijayo na tutaanza na Bandari."

Katika ripoti yake hiyo, CAG Charles Kichere, aliibua hoja ya kuwapo kwa viashiria vya vitendo vya ubadhirifu kwenye Bandari za Mwanza na Kigoma.

CAG anabainisha kuwa katika Bandari ya Mwanza Sh. bilioni 3.7 zilitolewa kwenye akaunti ya TPA iliyoko CRDB kupitia miamala 737 pasi na kuonyeshwa kwa hati za malipo na matumizi katika vitabu vya fedha.

Kwenye Bandari ya Kigoma, CAG anabainisha kuwa Sh. milioni 655.9 zilitolewa kutoka benki kwa kutumia hundi 30 bila kuwa na hati ya malipo kuthibitisha malipo yaliyofanywa na hundi hazikusajiliwa kwenye daftari la udhibiti wa hundi huku vipande vitano vya hundi vikikosekana kwenye daftari la udhibiti wala taarifa za benki.

"Nyaraka kama vitabu vya hundi, hati za uhamishaji fedha na taarifa za bodi ya zabuni hazikutolewa kwa uchunguzi zaidi," anabainisha.

Ripoti hiyo pia inabainisha ukosefu wa ripoti za mapato za kila siku ili kuhakiki ripoti za mapato ya kila mwezi kwa kipindi cha miezi saba.

Vilevile, CAG anabainisha kuwa mamlaka ilitumia viwango vya chini vya ushuru katika tozo za kushusha na kupakia mizigo kwenye meli (Stevedoring) na tozo za kutoa mzigo kutoka kwenye gati hadi kwa mteja (shore-handling) ambazo kwa pamoja zilitozwa Dola za Marekani nane badala ya 10.

Pia ilibainika tozo za maegesho ya meli katika eneo la bandari (Dockage/buoyage) zilitozwa Dola za Marekani 10 badala ya 15 kwa uingizaji na usafirishaji wa bidhaa nje, jambo ambalo ni kinyume cha tozo za bandari zilizopangwa kutumika katika bandari zilizopo katika maziwa zilizotolewa Januari 2018.

CAG pia alibaini TPA ilikodisha ardhi (Ukanda wa Bandari ya Mtwara) kwa EPZA mwaka 2014, kwa kipindi cha miaka 33 na ada ya kukodisha ya miaka 10 Dola za Marekani milioni 3.6 ilitakiwa kulipwa kabla.

Hata hivyo, anabainisha kuwa EPZA ililipa Dola za Marekani milioni 1.51 tu na Dola milioni 2.09 zilikuwa hazijalipwa.

"TPA pia ilikodisha ardhi (Bandari za Ndumbi) kwa TANCOAL Energy Limited (TEL) mwaka 2012. TEL ilitakiwa kulipa kodi kabla kila robo mwaka.

"Hata hivyo, hadi mwaka 2019/20, TEL haikuwa imelipa kiasi cha Sh. milioni 745.79 ambazo imelimbikiza tokea mwaka 2012," CAG anabainisha.

Wakati wa mkutano uliopita wa Bunge la Bajeti, Spika Job Ndugai, alitangaza kuwa mkutano ujao wa Bunge utakuwa mahususi kwa chombo hicho kushughulikia hoja zilizoibuliwa na CAG.

Ripoti ya CAG kwa mwaka 2019/20, iliwasilishwa bungeni Aprili mwaka huu.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Prof. Edward Hoseah, wakati ujumbe wa chama hicho ulipofika Ikulu Chamwino, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Gazeti la Uhuru lajifungia kwa upotoshaji kuhusu Rais

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ametangaza kufunga uzalishaji gazeti la Uhuru kwa siku saba na kuwasimamisha kazi viongozi watatu baaada ya kuchapisha taarifa za uongo dhidi ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Waliosimamishwa ni Mkurugenzi Mtendaji, Ernest Sungura, Mhariri Mtendaji Ramadhani Mbwaduke na Msimamizi wa toleo hilo, Rashid Zahoro.

Toleo la jana katika gazeti hilo lilikuwa na habari yenye kichwa kilichosomeka 'Sina wazo kuwania urais 2025- Samia', habari ambayo CCM imesema ni upotoshaji mkubwa wa kumlisha maneno Rais Samia.

Chongolo alitangaza uamuzi huo jijini Dar es Salaam jana alipozungumza na waandishi wa habari na kubainisha kuwa wamemkosea, Rais kwa kumlisha maneno ambayo hakusema na wanamwomba msamaha.

"Niliagiza bodi kukutana na tayari wamekutana na kuniletea taarifa ya hitimisho la kikao chao, jambo la kwanza bodi imechukua uamuzi kwa kuwasimamisha kazi viongozi ambao wameonekana kuhusika moja kwa moja kwenye shughuli la gazeti husika.

"La mwisho, mimi ndio Katibu Mkuu, nimesimamisha kuanzia leo (jana) uchapaji wa gazeti la Uhuru kwa siku saba, haya ni mamlaka yangu," alisema Chongolo.

Wakati uongozi wa CCM ukichukua hatua hiyo, serikali imetangaza kusitisha kwa wiki mbili leseni ya uchapishaji wa gazeti hilo kuanzia leo.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Gerson Msigwa, Mkurugenzi wa Idara ya Habari-MAELEZO, ameamua kuchukua uamuzi huo kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 9(b) cha Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya 2016, Alisema uamuzi wa kusitisha leseni ya uchapishaji na usambazaji wa gazeti hilo unatokana na gazeti hilo toleo Na. 24084 la jana katika ukurasa wa mbele kuchapisha habari inayosomeka 'Sina wazo kuwania urais 2025 - Samia'.

"Ofisi ya Mkurugenzi wa Idara ya Habari-MAELEZO, imebaini kuwa habari hiyo ina upungufu wa kisheria na weledi wa taaluma ya uandishi wa habari kwa kutoa taarifa za uongo dhidi ya Rais," alisema.

Katika mkutano wake wa jana, Chongolo aliwaambia waandishi wa habari kuwa, kumekuwa na tatizo la kutokupima mapema idadi ya wanafunzi wanaojiunga na darasa la awali, darasa la kwanza na kidato cha kwanza kila mwaka wa masomo.

Alisema CCM imeiagiza serikali kuhakikisha fedha za ujenzi wa miundombinu ya elimu ikiwamo madarasa, kutengwa kwenye robo ya mwaka, ili kufanya maboresho mapema badala ya kusubiria mwakani.

## 15 wafa kwa corona Zanzibar, 390 waugua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya wagonjwa wa corona Zanzibar imeongezeka kufikia 390, huku vifo vikiwa 15 ambavyo vilivyotokea katika hospitali mbalimbali.

Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema idadi hiyo ni kutoka Juni hadi Agosti mwaka huu.

Waziri Mazrui alisema kati ya hao 390 waliopata corona, Watanzania ni 112 na wageni kutoka ughaibuni 278.

"Kati ya watu 390 waliothibitika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona, 207 wamepona na wanaendelea na majukumu yao na wagonjwa waliobaki ni 183 (Watanzania 32 na wageni ni 151) na wagonjwa 24 wamelazwa na wanaendelea na matibabu katika hospitali mbalimbali Zanzibar," alisema.

Alisema kuanzia Juni 25 hadi Agosti 10 jumla watu 29,326 wamepimwa virusi vya corona katika vituo na hospitali mbalimbali Unguja na Pemba na miongoni mwao, watu 390 walithibitika kuwa na maambukizi ya virusi hivyo.

Aidha, alisema kati ya watu 390 waliothibitika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona, 207 wamepona na wanaendelea na majukumu yao na wagonjwa waliobaki ni 183 (Watanzania 32 na wageni ni 151) na wagonjwa 24 wanaendelea na matibabu.

Akizungumzia kuhusu chanjo ya corona, Mazrui alisema Wizara ya Afya inaendelea na hatua mbalimbali za kinga dhidi ya ugonjwa huo ukiwamo utoaji wa chanjo, na kwamba wameanza kutoa chanjo kwa makundi maalum ambayo ni hatarishi zaidi kuambukizwa.

Aliyataja makundi hayo ni wafanyakazi wa milango mikuu ya kuingia Zanzibar (viwanja vya ndege na bandarini), wadau wa utalii wakiwamo waongoza watalii, madereva wanaosafirisha wageni na watalii. Wamo pia wafanyakazi wa vyombo vya usafiri vya ndani na nje ya nchi, wafanyakazi wa mahoteli, wazee kuanzia miaka 55 na watu wenye magonjwa sugu na ya muda mrefu.

# Mawakili wa Sabaya wagonga mwamba

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imetupilia mbali pingamizi la mawakili wa utetezi kutaka ushahidi wa nyaraka, picha tano za mnato, barua na baadhi ya nyaraka kupokelewa kama sehemu ya vielelezo vya ushahidi katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake wawili.

Mbali na Sabaya (34), washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38). Wote wanakabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Akitoa uamuzi mdogo, Hakimu Mkazi Mwandamizi Odira Amworo, alisema vielelezo hivyo ni sahihi kupokewa mahakamani.

Juzi, Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, alipinga vielelezo hivyo kupokelewa mahakamani kwa madai kwamba, utaratibu wa kisheria wa kuwasilishwa haukufuatwa.

Hoja hiyo ilipingwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, kwa madai kwamba vinapaswa kupokelewa kwa kuwa vinaonyesha uhalisia na kuithibitishia mahakama mlalamikaji, Bakari Msangi, alivyoshambuliwa katika maeneo mbalimbali.

Katika hatua nyingine, shahidi wa 11 wa Jamhuri, ambaye ni mpelelezi wa kesi hiyo, Konstebo James (31), jana aliendelea kutoa ushahidi wake.

Kachero huyo wa Jeshi la Polisi, akiongozwa na Kweka, alionyesha vielelezo vya picha tano mahakamani, zikionyesha Bakari Msangi, akiwa amevimba kwenye mashavu, masikio na kuvilia damu pamoja na alama za vidole baada ya tukio la kudaiwa kupigwa na Sabaya katika duka la Shahidi Store.

Shahidi huyo alidai kwamba vielelezo vinavyotakiwa kupokelewa, vinaonyesha tukio la kushambuliwa kwa Msangi, uchunguzi wa majeraha ya malalamikaji ulifanyika katika Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi (CFB).

"Mlalamikaji alipokwenda Hospitali ya Mount Meru kwa ajili ya kupata matibabu, tulimpiga picha tano na kuzituma Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi, ili kuithibitishia mahakama kwamba mlalamikaji alipigwa na kushambuliwa na Sabaya na walinzi wake.

Shihidi huyo aliwasilisha mahakamani picha tano, barua na baadhi ya nyaraka zikionyesha kwamba picha hizo zilifanyiwa kazi na kamisheni hiyo ya uchunguzi.

Kachero huyo, alidai kwamba walibaini kupitia uchunguzi wao kuwa mbali na Msangi kupiga, kutekwa nyara na kuwaweka chini ya ulinzi, pia alipokonywa Sh. 390,000. Pia alidai kwamba Msangi, Numan na wenzake walitishitiwa bastola, Sabaya alipovamia duka hilo.

Shahidi huyo pia, alidai kwamba Sabaya na walinzi wake, walipora Sh. 276,900 katika duka la Mohamed Saad, siku ya tukio Februari 9, mwaka huu na kwamba Februari 14, washtakiwa walipokamatwa na kuhifadhiwa kituo cha polisi, aliwatambua watu watatu, ambao ni Sabaya, Mbura na Deogratius Prosper.

Alidai kwamba alianza kazi ya kupeleleza jalada hilo Februari 12 majira ya saa 11:00 jioni, akiwa ameambatana na Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Wilaya (OC-CID) na makachero wengine, pamoja na Numan Jasin, kwenda kufanya upelelezi katika duka hilo.

"Tulipofika katika eneo hilo, Numan, alifungua duka kwa ajili ya sisi kuanza kufanya upelelezi wa tukio hilo. Na wakati tukiingia dukani huko, tulikuta vitu vikiwa vimesambaratika na pembeni ya kaunta kulikuwa na maji maji na matone ya damu yaliyoganda,

"Nilimuuliza Numan maji yale yalitoka wapi na kutueleza kuwa mmoja wa vijana aliyekuwa dukani alijikojolea. Pia wakati tukikangua kutaka kupata uhalisia wa tukio hilo kwenye CCTV Camera, tulibaini 'footage' zilichezewa." Alidai.

Shahidi huyo alidai kwamba walibaini kwamba kamera hizo zilichezewa kwa kugeuzwa kwa kuwa baada ya kuwahoji wahusika, waliwaeleza hazikuwa katika uelekeo wake wa siku zote.

James alidai kwamba wakati wanamhoji Numan, aliwaeleza kwamba Sabaya na walinzi wake, waliwashambulia kwa kuwapiga ngumi, mateke na vibao ndipo walibaini kwamba kuna kitendo cha jinai kilifanyika dukani huko.

"Watu waliopigwa kwenye tukio ni Hajirini Saada, Numan Jasin na Bakari Msangi na kwa mujibu wa mwathirika wa tukio hilo walipigwa na walinzi wa Sabaya wakishinikiza kuambiwa sehemu alipokuwa mmiliki wa duka," alidai shahidi huyo.

# AU kuipa Tanzania dozi milioni 17 chanjo corona

**Na Mwandishi Wetu,** ADDIS ABABA

UMOJA wa Afrika umeitengea Tanzania dozi milioni 17 za chanjo za UVIKO- 19 kupitia mpango wa umoja huo wa kuzisaidia nchi wanachama kupata chanjo kwa ajili ya wananchi wake.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, aliyasema hayo Addis Ababa, Ethiopia jana alipokutana kwa mazungumzo na Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Ethiopia waliotaka kufahamu hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali katika kupambana na UVIKO-19 ikiwa ni pamoja na suala la chanjo.

Balozi Mulamula aliwataka Watanzania wanaofanya kazi katika mashirika na taasisi mbalimbali za kimataifa, kusaidia upatikanaji dozi nyingine za chanjo ya UVIKO-19, ili kuwawezesha Watanzania wengi kupata chanjo hiyo kutokana na mwamko wa Watanzania baada ya kuzinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Katika tukio lingine, Waziri Mulamula alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Ethiopia, Sahle - Work Zewde, Tanzania na Ethiopia zimekubaliana kuendelea kutumia ndege za Shirika la Ethiopia kutangaza vivutio na kusafirisha watalii kutoka mataifa mbalimbali kwenda Tanzania.

Balozi Mulamula alimhakikishia Rais Zewde kuwa Tanzania itaendelea kutekeleza maeneo yote ya ushirikiano ambayo Rais Zewde alikubaliana na Hayati Dk.John Pombe Magufuli wakati wa ziara ya Rais huyo Chato, ikiwa ni pamoja na suala la kuwarejesha Ethiopia wahamiaji wanaoshikiliwa katika magereza mbalimbali.

Rais wa Ethiopia, Zewde alisisitiza kuendelea kuimarisha ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na nchi hiyo hususani katika kutatua kero zinazozuia maendeleo kati ya mataifa hayo.

# Musiba aamriwa kumlipa Fatma Karume bil. 7.5/-



**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Zanzibar imemwamuru Cyprian Musiba na Gazeti la Tanzanite, kumlipa fidia ya Sh. bilioni 7.5, Fatma Karume (Pichani) baada ya kubaini alimchafua kwa kumzushia taarifa za uongo.

Uamuzi huo ulitolewa jana baada ya mahakama hiyo iliyoko Vuga kusikiliza madai ya Fatma dhidi ya Musiba na hoja za utetezi zilizowasilishwa na mlalamikiwa huyo.

Fatma aliyekuwa Wakili wa Kujitegemea, alifungua kesi mwaka 2019 dhidi ya Musiba akilalamikia kuchafuliwa na mara ya kwanza ilitajwa Oktoba 3, 2019.

Katika madai yake, Fatma alimlalamikia Musiba kwa kumchafua kwa kumzushia taarifa za uongo zenye lengo la kushusha hadhi yake katika jamii.

Fatma anadai katika malalamiko yake kwamba, Musiba alimwambia ametiwa mimba na muuza unga na kwamba hana staha wakati anadai maelezo hayo si kweli kwa kuwa ana mume na watoto.

Katika kesi hiyo, Fatma alikuwa akiwakilishwa na Wakili Karume Mrisho ambaye alidai jana, kuwa mteja wake kwa sasa yuko nje ya nchi.


The Guardian Limited

VACANCY

Freelance Sales Executives

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.**

61637602

# Vigogo wa NIDA wana kesi ya kujibu

**Na Hadija Kitwana**

ALIYEKUWA Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Dickson Maimu na wenzake wanne, wamekutwa na kesi ya kujibu katika mashtaka yanayowakabili ya matumizi mabaya ya madaraka.

Uamuzi huo ulitolewa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kisutu na Hakimu Mkazi Mwandamizi Rashidi Chaungu baada ya Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladislaus Komanya, kudai kuwa shauri hilo lilikuja kwa ajili ya uamuzi kama washitakiwa wanakesi ya kujibu au la.

Akiwasilisha hoja hiyo, Komanya alidai kuwa upande wa mashitaka uko tayari na hatimaye upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili George Ndunguru, nao ulidai uko tayari.

Hakimu Chaungu, akitoa uamuzi huo, alisema washtakiwa wanakabiliwa mashtaka 55, ambayo ni kuongoza genge la uhalifu (shtaka moja), kughushi (mashtaka saba) na matumizi mabaya ya madaraka (shtaka moja).

Mengine ni kusababisha hasara kwa mamlaka (makosa sita), utakatishaji fedha (makosa 10), kutoa hati ya uongo (makosa matatu) na makosa 25 ya kumdanganya mwajiri.

Hakimu Chaungu alisema washtakiwa wote walikana makosa hayo na upande wa mashitaka ulipeleka mashahidi 26 na vielelezo 45 na kwamba amepitia ushahidi, ameridhika kwamba wote wana kesi ya kujibu na watajitetea kwa kiapo au la na je, watakuwa na mashahidi wangapi.

Baada ya Hakimu Chaungu kusoma uamuzi pande zote mbili ya utetezi na mashtaka zilikubaliana na uamuzi huo.

Upande wa utetezi ukianza na mshtakiwa namba moja, Mwaimu, ulidai kuwa atajitetea kwa kiapo na ataleta mashahidi si chini ya 20 na vielelezo si chini ya 10 na mshtakiwa wa pili, Xavery Kayombo, alidai kuwa atajitetea kwa kiapo ana mashahidi watano na yeye wa sita na vielelezo hajajua atapeleka vingapi.

Mshitakiwa wa tatu, Aveln Momburi, alidai atajitetea kwa kiapo na ataleta mashahidi wasiopungua watano na vielelezo visivyozidi 10 huku mshitakiwa namba nne, George Ntalima, alidai kuwa ataleta mashahidi wasiopungua wanne na vielelezo visivyozidi vitatu.

Kwa upande wake, mshitakiwa wa tano, Sabina Raymond, alidai atajitetea kwa kiapo na mashahidi wasiozidi wawili na vielelezo visivyozidi sita.

Baada ya upande wa washtakiwa kumaliza kujielezea, Hakimu Chaungu aliahirisha kesi hadi Agosti 25 na 26, mwaka huu, kwa ajili ya kusikilizwa kwa ushahidi upande wa utetezi.

Maimu na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 25 likiwamo la kuisababishia hasara serikali ya Sh. bilioni 1.175.




Jaji Mstaafu Robert Makaraba (kushoto), akimwapisha Mwanahabari Mwandamizi Selemani Mpochi kuwa Jaji kati ya majaji saba wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2020, walioapishwa katika ofisi za Baraza la Habari Tanzania (MCT), mkoani Dar es Salaam jana. Katikati ni Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Kajubi Mukajanga **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tuzo za EJAT kutolewa kidigitali

**Na Elizabeth Zaya**

KILELE cha Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa Mwaka 2020 zitafanyika mwezi ujao kwa njia ya mtandao.

Akizungumza baada ya kuapishwa kwa jopo la majaji wa tuzo hizo jana, mkoani Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT Mwaka 2020, Kajubi Mukajanga, alisema kilele cha tuzo hizo ni Septemba 10, mwaka huu.

"Kilele cha Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania Mwaka 2020 kitafanyika kwa njia ya mtandao, wadau wote wa habari watapatiwa 'link' kwa ajili ya kushiriki katika sherehe za tuzo hizo.

"Hii ni mara kwanza tuzo hizi kufanyika kwa njia ya mtandao kutokana na masharti ya ugonjwa wa UVIKO-19.

"Kwa hiyo, kutakuwa na kituo maalum ambacho kitakuwa kinatangaza tuzo hizo na waalikwa watakuwa ni wachache sana wakiwamo majaji, wafadhili, washirika wetu na waandishi wa habari".

"Washindi wote watakaotangazwa watachukua zawadi zao, katika ofisi za MCT kwa waliopo Dar es Salaam na kwa walioko mkoani watatumiwa," alifafanua.

Mukajanga ambaye ndiye Katibu Mtendaji wa MCT, alisema majaji hao walioapishwa jana wanatarajia kuanza kazi leo na wataifanya kwa muda wa wiki moja.

Alibainisha kuwa jumla ya kazi 395, ziliwasilishwa kutoka kwa waandishi wa habari nchi nzima kwenye vipengele 19, vinavyoshindanishwa katika tuzo hizo. Kati yake, 77 ni washiriki wanaume na 70 ni wanawake na kufanya jumla ya washiriki kuwa 147.

"Kati ya kazi 395 zilizowasilishwa, 59 zilitoka Dar es Salaam, Pemba 27, Unguja 24, Mwanza 22 na Dodoma 21.

"Vyombo vya kielektroniki ndivyo vinavyoongoza kwa kuwasilisha kazi nyingi, vikifuatiwa na magazeti pamoja na zile za mtandaoni," alisema Mukajanga.

Akizungumza baada ya kuwaapisha majaji hao, Jaji mstaafu Robert Makaramba aliwataka majaji wa tuzo hizo kufanya kazi hiyo kuwa uaminifu na kwa kutenda haki.

"Ninachoweza kuwaambia ni kwamba ni vyema mkazingatia kufanya kazi hii mliyopewa kwa uaminifu na kuhakikisha kwamba mnatenda haki kwa anayestahili, kwa sababu tukio kama hili halina kukata rufani, haki ya wale mnaoenda kufanya kazi zao iko mikononi mwenu" alisema Jaji Makaramba.

Jopo la majaji wa tuzo hizo walioapishwa jana linaongozwa na Mwenyekiti, Dk. Joyce Bazira, na Katibu wao ni Imane Duwe.

Wajumbe wa jopo hilo ni Dk. Egbert Mkoko, Selemani Mpochi, Masoud Ally, Mkumbwa Ally na Lucas Liganga.

## Wafungwa miaka 25 kusafirisha binadamu

**Kulwa Mzee na Hadija Kitwana**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewatia hatiani na kuwahukumu kwenda jela miaka 25 washtakiwa watatu kati ya watano wanaotumiwa kufanya biashara haramu ya kusafirisha binadamu.

Washtakiwa hao wanadaiwa kusafirisha raia wa Tanzania 90 na raia wa Burundi watano kwenda Canada na Mauritania.

Hakimu Mkazi Mfawidhi, Godfrey Isaya, aliwatia hatiani washtakiwa hao Ally Rajabu, Arnold Ssali na Chebet Benson, baada ya kukiri makosa yanayowakabili.

Mahakama ilimhukumu Ally kwenda jela miaka 20 au kulipa faini ya Sh. milioni 20 na mshtakiwa Ssali na Chebet, wamehukumiwa kwenda jela miaka mitano au faini ya Sh. milioni 10.

Washtakiwa Mohammed Shalabi ambaye ni raia wa Misri na Fikirini Makubi wanaendelea na mashtaka yanayowakabili na leo watasomewa maelezo ya awali dhidi ya mashtaka yao.

Kabla ya kufikia hatua hiyo Wakili wa Serikali, Godfrey Ngwijo, aliomba kuwasomea washtakiwa hati mpya ya mashtaka kwa kuwaongeza washtakiwa wawili ambao awali hawakuwapo.

Walioongezwa katika kesi hiyo ni Mkurugenzi wa Hospitali ya Kimataifa ya Ssali, Arnold Ssali ambaye ni raia wa Uganda na Mtanzania, Fikirini Makubi.

Katika hati mpya mshtakiwa wa kwanza Mohammed anadaiwa Agosti 4, mwaka huu, katika makazi ya Avone wilayani Ilala akiwa raia wa Misri na Mauritania alikutwa akisafirisha watu 95 wakiwamo Watanzania 90 na raia wa Burundi watano kwenda Canada na Mauritania.

Katika shtaka la pili mshtakiwa Ally na Fikirini katika kipindi hicho wanatuhumiwa kujihusisha na mpango wa biashara haramu ya kuuza binadamu.

Shtaka la tatu kwa mshtakiwa Ssali anatuhumiwa kuajiri raia wa kigeni bila kuwa na kibali na Agosti 4, mwaka huu akiwa mkurugenzi wa hospitali hiyo alimwajiri Chebet ambaye ni raia wa Uganda wakati hana kibali, alikubali kutenda kosa.

Mshtakiwa Chebet anatuhumiwa kufanya kazi nchini bila kibali kosa ambalo alikiri.

Baada ya mshtakiwa Ally, Ssali na Chebet kukiri makosa yao, Mahakama iliwatia hatiani na kuwapa nafasi ya kujitetea na katika utetezi wao walidai ni wakosaji wa mara ya kwanza, wana wazazi wanawategemea waliomba wapunguziwe adhabu.

Baada ya kusikiliza hoja hizo mahakama ilimuhukumu mshtakiwa Ally kwenda jela miaka 20 au faini ya Sh. milioni 20.

Pia ilimhukumu mshtakiwa Ssali na Chebet kwenda jela miaka mitano au kulipa faini Sh. milioni 10, wote walikwenda jela.

Mshtakiwa Mohamedi na Fikirini waliobakia kesi yao imepangwa leo kwa ajili ya kusomewa maelezo ya awali.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Viongozi vyama vya siasa wahamasishe chanjo corona

**IMERIPOTIWA** kuwa 126 wamepatiwa chanjo corona wilayani Njombe Mkoa wa Njombe kuanzia Agosti 5, mwaka huu, tangu uzinduzi wa chanjo ufanywe na Rais Samia Suluhu Hassan, mwishoni mwa mwezi uliopita.

Idadi hiyo ya watu waliochanjwa, ni kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Dk. Stanley Mlay na kwamba ili kuongeza kasi ya uchanjaji, halmashauri hiyo imeamua kuongeza vituo vyingine vinne kutoka vitatu vilivyokuwapo awali.

Anasema mwitikio ni wa wastani, tangu waanze kutoa chanjo, na kutoa wito kwa walengwa wa chanjo hiyo kujitokeza kwa wingi ili kuchanjwa kwa kuwa ni salama.

Kwamba huduma hiyo ni salama, kwa sababu serikali ipo inazisimamia, na kushauri watu kujitokeza kwa wingi ingawa suala la chanjo ni hiari, lakini ni muhimu kwa ajili ya kupunguza matatizo ambayo yanaweza yakatokea.

Wakati huduma ya chanjo ikiendelea kutolewa katika maeneo mbalimbali nchini, tunadhani kwamba kuna haja kwa wadau wote kushiriki kwenye kazi ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kuliko ilivyo sasa.

Tunataja wadau kwa maana ya viongozi wa vyama vya siasa, kwamba wao pia wanaweza kushiriki katika uhamasishaji ili Watanzania wengi zaidi waendelee kujitokeza kuliko ilivyo sasa. Mfano mzuri ni hiyo idadi ya watu wa wilaya ya Njombe, ambayo kimsingi ni ndogo hasa ikizingatiwa kwamba wilaya inaundwa na vijiji vingi, hivyo kujitokeza watu 126 tunadhani ni idadi ndogo.

Sisi tunashauri wanasiasa kama wadau washiriki katika uhamasishaji, kwa sababu, kwanza wana majukwaa ya kukutana na wanachama wao ikiwamo vikao vya ndani na hata mikutano mingine, ambayo wanaweza kuitumia pia kwa kazi hiyo. Viongozi wa vyama vya siasa, ni miongoni mwa Watanzania ambao wamepata chanjo na wakakiri kuwa haina matatizo, hivyo kwa kauli zao hizo, tunadhani ni vyema wakazitumia pia kushawishi wanachama wakachanjwe.

Kwa kutumia ushawishi wao wa kisiasa, tunaamini idadi ya watu kujitokeza kuchanjwa inaweza kuongezeka, ingawa kuchanjwa ni hiari, lakini wakati mwingine watu hawajitokezi kutokana na ukosefu wa elimu sahihi kuhusu chanjo.

Pamoja na kwamba viongozi hao wanaweza kuwa na majukumu mengi, lakini tunaona kuwa si vibaya ndani ya majukumu hayo wakaongeza lingine la kuwaelekeza wanachama na umma kwa ujumla kupata chanjo ili nao wawe salama.

Kwa kuwa wao wameshachanjwa, tunaona kwamba, wana nafasi nzuri ya kuwahakikishia usalama wa chanjo hiyo wanachama wao ambao bado wanasita kuchanjwa kutokana na sababu mbalimbali. Tunadhani kwamba kusuasua kwa wananchi kujitokeza kuchanjwa katika maeneo kadhaa ya nchi yetu, kunaweza kuchangiwa na mambo mawili, uhiari na kutokana na elimu waliopewa awali.

Hivyo, sisi kwa mtazamo wetu ni kwamba, wadau hasa viongozi wa vyama vya siasa kwa kutumia majukwaa yao, wana nafasi nzuri ya kuwaeleza wale ambao wanasita kujitokeza kwa sababu ya elimu ya awali waliopata kuhusu chanjo pengine kutowafikia wengi.

Tumetoa msisitizo kwa wanasiasa tikiamini kwamba nyuma yao kuna watu wengi ambao ni wafuasi wao, ambao ni rahisi kuwasikiliza na kuwaamini.

Kwa upande mwingine, kuna viongozi wa dini ambao nao wana wafuasi wengi nyuma yao. Hata hivyo, jambo la kufurahisha wamekuwa mstari wa mbele wa kuwahamasisha na kuwashawishi waumini wa dini zao kupata chanjo hiyo tangu siku iliyozinduliwa na Rais Samia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

### Mbinu chafu zisipewe nafasi vyeti chanjo corona

**CHANJO** ya kujikinga na ugonjwa wa corona, inayoendelea kutolewa kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini, baada ya kuzinduliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa mwezi uliopita.

Hadi kufikia Agosti 7, mwaka huu, zaidi ya Watanzania 164,500 walikuwa wameshajiandikisha kwa ajili ya kupatiwa chanjo wiki hii, huku wengine 105,745 wakiwa tayari wameshachanjwa.

Katibu wa Wizara yenye dhamana na Afya za Watanzania, Profesa Abel Makubi, anatoa taarifa hiyo na kufafanua kuwa baada ya uzinduzi, utoaji wa chanjo ulikuwa umefika mikoa yote Agosti 4, mwaka huu.

Pamoja na kutoa takwimu hizo, katibu huyo anatoa tahadhari iwapo kuna watu watakaojaribu kujipatia vyeti vya chanjo kwa njia za udanganyifu, kuwa watakaobainiwa na mfumo watachukuliwa hatua za kisheria.

Inawezekana amefikia kutoa tahadhari hiyo kutokana na kwamba baadhi ya watu huwa wanapenda kufanya mambo kwa mkato bila kufuata taratibu, hivyo anaona kuna haja ya kuwatahadharisha.

Hata hivyo, inaweza kushangaza watu kufikia kufanya udanganyifu kwenye chanjo wakati maelekezo ni kwamba kuchanjwa ni hiari. Kama ndivyo, ninadhani itakuwa si sahihi kutafuta vyeti vya chanjo kwa njia hiyo.

Waswahili wana msemo wao kwamba, lisemwalo lipo, kama lipo laja, hivyo inawezena katibu huyo amebaini kuwapo kwa ujanja huo au kuna mbinu zinaendelea kufanyika ili watu wajipatie vyeti vya chanjo bila kuchanjwa.

Kwa mujibu wa maelekezo ya serikali, kila mtu ana hiari ya kuchanjwa au kutochanjwa, hivyo ingependeza kama mtu ambaye hataki kuchanjwa kabaki nyumbani ili wengine waendelee kupata huduma hiyo.

Kimsingi suala la chanjo ni la hiari, kwa hiyo si vibaya mtu aamue moja, kwenda kupata chanjo au kutochanjwa, ili kuepusha kuwapo kwa taarifa za kuwapo kwa njia nyingine za kusaka vyeti bila kuchanjwa.

Wizara inakumbusha inafahamu mfuatano wa namba zake na zimetolewa kituo gani, hivyo, ikitokea namba moja imejirudia uchunguzi utaanzia kwa watoa huduma waliotoa namba hizo na wateja wenye vyeti vya namba hizo.

Kauli hiyo inaonyesha kuwa kuna haja kwa watoa chanjo na wale wanaochanjwa kuzingatia maelekezo ya serikali, ili kuepuka kuingia kwenye mtego ambao unaweza kusababisha wachukuliwe hatua za kisheria.

Muungwana anaunga mkono maelekezo na wito wa serikali kwa watoa huduma ya chanjo na wapokea huduma, kwani anaamini kuwa kila mmoja kutimiza wajibu wake, hakutakiwa na mbinu nyingine zisizofaa.

Ikumbukwe, kinachosisitizwa, ni watoa huduma kutogeuza chanjo kwa namna yoyote kuwa kama biashara, badala yake kazi ifanyike kuhakikisha wanaofika kwenye vituo wanapata huduma inavyotakiwa.

Wizara inawakumbusha kuwa kadi maalumu za kielektroniki zinazoendelea kuandaliwa, na kwamba zitakuwa na vigezo vya kimataifa vya uthibitisho wa kupata chanjo, mojawapo ya vigezo hivyo vikiwa ni utambulisho wa siri .

Utambulisho huo utajumuisha taarifa za mpokeaji chanjo, chanjo aliyopata, muda na mahali alipochanjwa, na kadi hizo zitatolewa kwa kila waliochanja hata ambao kwa sasa wamepewa cheti cha nakala ngumu watafikiwa kupewa cheti kipya kitakachosomeka kwenye mfumo wa kielektroniki.

Kwa utaratibu huo, ni wazi kwamba wale ambao wanajipanga kufanya usanii katika chanjo kwa lengo la kujipatia chochote, ni bora wakaacha na mawazo hayo na kuamua moja, wachanjwe au wasichanjwe.

Lakini wakumbuke kuwa msisitizo wa serikali kwenye suala la chanjo kwamba ni hiari ya mtu, hivyo anayelazimishwa kwenda kuchanjwa na pia wahudumu nao wakumbuke kuwa chanjo ya corona inatolewa bure.

Aidha, taratibu zikifuatwa, ninaamini kwamba, serikali itapata takwimu sahihi za watu waliochanjwa, badala ya kuwapo mbinu ambazo zinaweza kusababisha kuwapo na idadi waliochanjwa ambayo si halisi.

# W'biashara wakimbia soko, waingia mtaani

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WANYABIASHARA wadogo maarufu kama Machinga katika Soko la Kiloleli, Manispaa ya Ilemela, jijini Mwanza wametelekeza vibanda vyao katika soko hilo na kuingia mtaani.

Diwani wa Kata ya Ibungilo, Hussein Magera, alisema kero wanazokumbana nazo ni pamoja na ubovu wa miundombinu ikiwamo vyoo, kutokamilika kwa soko pamoja na stendi.

Alisema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari katika soko hilo jijini hapa.

"Machinga wamelitelekeza soko hili kwa sababu ya miundombinu hafifu, choo ni kimoja hakiwezi kuhimili wafanyabiashara wote, mazingira pia siyo rafiki kama mvua inaponyesha na wakati wa jua," alisema Magera.

Alisema halmashauri ilisema imetenga kiasi cha Sh. milioni 82 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo, lakini mpaka sasa wameshindwa kukamilisha kazi hiyo.

Vile vile, alisema anamshukuru Mkuu wa Wilaya ya Ilemela pamoja na mkurugenzi wake kwa kufanya ziara katika soko hilo na kuahidi kutatua kero za wafanyabiashara hao.

"Jukumu langu kama diwani nitahakikisha nasimamia ujenzi wa miundombinu rafiki katika soko hili la wilaya na mambo yanaenda vizuri kwani tumetoka kwenye kikao na Mkuu wa Wilaya na tumejadili kuhusiana na mradi huu," alisema.

Alisema miundombinu ya soko hilo itaanza kuboreshwa kuanzia mwezi wa 10 na kukamilika mwezi wa 12 na kuwataka wafanyabiashara wadogo kurudi katika soko hilo.

Kwa upande wake, mwenyekiti wa wafanyabiashara wadogo katika soko la Kiloleli, Modest Simfukwe, alisema Mkuu wa Wilaya ameonyesha nia ya kukamilisha miundombinu hiyo ili wafanyabiashara waepuke adha za mvua.

# Waomba kulegezwa masharti ya takwimu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI imeombwa kulegeza masharti yaliyomo kwenye Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2019 yanayombana mwandishi wa habari katika matumizi ya takwimu ili kuboresha kazi yake na huduma zake kwa jamii.

Hayo yalisemwa jana kwa nyakati tofauti na washiriki wa mafunzo ya uandishi wa habari na wadau wa habari mkoani hapa yaliyoandaliwa na Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (MISA -TAN) na IMS chini ya ufadhili wa Shirika la Misaada la Umoja wa Ulaya (EU Action).

Walisema kubanwa kwa takwimu hizo kunawafanya wanahabari kukosa kuandika habari au makala kwa upana zaidi na kuuelewesha umma.

Mmoja wa washiriki hao, Vumilia Kondo, alisema sheria hiyo inabana uhuru wa habari hasa pale mwanahabari anapotaka kutumia takwimu hasa za masuala ya afya na kukuta zimeandikwa "usizitangaze" wakati kwa matumizi ya takwimu hizo mwandishi anaweza kutoa makala elekezi kwa jambo fulani kwa jamii.

Alisema wanahabari au taasisi za kijamii wanayo nafasi ya kukusanya taarifa zenye kuambatana na takwimu lakini sheria hiyo bado inawabana katika matumizi jambo ambalo si sahihi na kwamba matumizi ya takwimu hizo yangeruhusiwa na kuangaliwa baadaye kama yatakuwa na athari yoyote.

Kondo alisema kulegezwa kwa masharti hayo kutasaidia wanahabari kuandika habari zenye uthibitisho ambao ni takwimu baada ya kuzipata na kuujulisha umma yale ya muhimu yanayokusudiwa.

Kutokana na hali hiyo, washiriki hao waliiomba Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuweka usawa wa wanahabari au taasisi za habari na serikali wakati wa kuundwa kwa bodi ya ithibati kwa wanahabari ili kuwafanya kupata watu wa kuwazungumzia pale inapobidi.

Mdau wa habari na mkurugenzi wa asasi isiyo ya kiserikali inayojihusisha na masuala ya wanawake na jamii, Lusako Mwakiluma, alisema kuanzishwa kwa bodi hiyo bila kuzingatia uwapo kwa wanahabari kutawafanya kukosa pa kusemea baada ya serikali kuwa na nguvu zaidi ya kuzungumzia masuala ya wanahabari.

Naye mwezeshaji wa mafunzo hayo, Wakili Mohamed Tibanyendera, alisema Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 ambayo baadhi ya vipengele vyake bado havijaanza kutumika, imeonyesha kuapo kwa vikwazo kwa wanahabari.

Alisema utafiti uliofanywa na MISA-TAN unaonyesha kwamba uundaji wa bodi ya ithibati utakaofanywa na serikali hautawasaidia wanahabari kama hautazingatia kuwa na baadhi ya wanahabari au taasisi za habari ndani yake.

Tibanyendera pia alisema kulegezwa kwa masharti ya Sheria ya Takwimu yaliyomo kwa sasa yanayomnyima haki mwanahabari na mdau wa habari kutumia takwimu hadi ziwe zimethibitishwa, hakutakuwa na maana katika ushirikishwaji wa masuala ya kijamii yanayofanywa na wanahabari na wadau wa habari.

Alisema upatikanaji wa habari ni suala la kisheria na kwamba taarifa zinazotolewa kwa umma zinapaswa ziwe nyingi kuliko zinazobanwa kwa mujibu wa sheria na kwamba taarifa za mabadiliko ya sheria yoyote zinapaswa kuwekwa wazi pale tu zinapotungwa ili kusaidia wahusika kufanya kazi kwa ufanisi.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (katikati), akiwa na Meya wa Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila (kulia kwake), pamoja na Katibu wa CCM wilaya hiyo, Agnes Bashemu, wakiangalia mradi wa ufugaji nguruwe ambao unaendeshwa na kikundi cha watu wenye ulemavu Kitangili, Mjini Shinyanga, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Waziri Chamuriho ambana mkandarasi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Dk. Leonard Chamuriho, ameibana kampuni ya Gemen anayejenga barabara ya Kuseni hadi Suguti mkoani Mara yenye urefu wa kilomita tano kwa kiwango cha lami.

Dk. Chamuriho alifikia hatua hiyo baada ya mkandarasi huyo kusuasua katika utekelezaji wa kazi hiyo, hivyo kumtaka ahakikishe anakamilisha barabara hiyo haraka kama ilivyo kwenye mkataba.

Chamuriho alitoa agizo hilo jana wakati akikagua mradi huo ambao unatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 8.2 na kutarajiwa kukamilika Desemba, mwaka huu, lakini utekelezaji wake hauridhishi.

Sambamba na agizo hilo, Chamuriho alimpa mkandarasi huyo siku 14 kulipa madai ya mishahara ya zaidi ya wafanyakazi 30, ambao wanadai kutolipwa mishahara kwa miezi minane hali inayosababisha kushindwa kujikimu kimaisha.

"Mkandarasi hakikisha unamaliza mradi huu haraka kama ilivyo kwenye mkataba. Kasi mlio nayo bado haijaniridhisha. Pia hakikisha unawalipa wafanyakazi wako mishahara yao ndani ya siku 14," alisema.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Mara, Mhandisi Ngaile Mlima, amesema tayari Mkandarasi huyo ameshalipwa malipo ya awali ya kazi hiyo, hivyo hakuna sababu ya kutokumaliza kazi kwa wakati.

Alizitaja kazi zilizofanyika ni pamoja na kujaza changarawe, ujenzi wa tabaka la chini la barabara, ujenzi wa miundombinu ya maji na makalvati saba kati ya manane. Mhandisi Mlima aliongeza kuwa kazi zinazotarajiwa kufanyika sasa ni ujenzi wa tabaka la kati na la juu la barabara pamoja na ujenzi wa lami ya juu ya barabara na kwamba zitaanza mara moja kuanzia sasa.

Naye Issa Sikonya, mmoja wa wafanyakazi wa kampuni hiyo, alilalamika mbele ya Waziri Chamuriho kuwa Mkandarasi anasuasua kuwalipa mishahara, hivyo wanashindwa kupata hata hela ya kula.

Waziri Chamuriho yuko katika ziara ya kikazi mkoani Mara, pamoja na mambo mengine, alikagua miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa barabara ya Kuseni hadi Suguti.

# Makandarasi waonywa ukadiriaji wa gharama

**Na Joseph Mwendapole,**
MOROGORO

MAKANDARASI wametakiwa kuacha kuomba zabuni kwa gharama za chini, ili kuwavutia watoaji wa kazi kwa kuwa uzoefu unaonyesha wamekuwa wakishindwa kuzikamilisha na wengine kukimbia baada ya kuzipata.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Mhandisi Consolata Ngimbwa, wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa makandarasi wazalendo.

Alisema baadhi ya makandarasi wamekuwa wakijaza fedha ndogo kama mbinu ya kushinda zabuni lakini wanapopata kazi hizo, wanashindwa kuzikamilisha kwa wakati na wengine kushindwa kuzikamilisha kabisa.

"Jazeni zabuni vizuri tena kwa uhalisia. Msijaze tu ilimpate zabuni, lakini mwishowe zinawashinda. Hapa katikati tuliyumba sana baada ya serikali kuanza kufanya kazi zake kwa kutumia utaratibu wa 'force account' lakini sasa tumeanza kupata kazi za serikali. Tusifanye makosa, tuzifanye kwa weledi mkubwa," alisema.

Ngimbwa alisema CRB iliamua kuanza kutoa mafunzo hayo kwa makandarasi baada ya lawama nyingi kwamba, baadhi wamekuwa wakiweka bei ambazo hazina uhalisia wakati wa hatua ya zabuni.

Mhandisi Ngimbwa aliwasisitiza pia kufanya kazi kwa ubia na makandarasi wenzao na wanaposhindwa kujua namna ya kuzifanya wafike ofisi za bodi hiyo au kwa wataalamu, kwa ajili ya kuelekezwa namna ya kufanya kazi za aina hiyo.

"Wengi tunaingia kwenye kazi za ubia, lakini tunashindwa sijui kwa sababu hatuzijui au? Uzuri wa kazi hizi ni kwamba mnaunganisha nguvu na kufikia vigezo vinavyohitajika na kama mnashindwa njooni CRB mtaelekezwa," alisema.

Pia, aliwasisitiza makandarasi wazalendo kuungana na kuwa na chama kimoja chenye nguvu ambacho kitakuwa sauti yao wanapokuwa na shida za kuwasilisha serikalini.

Alisema watu wa tasnia mbalimbali kama wahandisi, wasanifu majengo, wakadiriaji majenzi na hata waendesha boda boda wanavyama vyao ambavyo vina nguvu.

"Kila siku tunazungumzia suala hili hili sijui tumekwama wapi sasa naomba ifike wakati tuseme inatosha, muwe na chama chenu chenye nguvu tusiwe tunazungumza jambo hili hili kila tukikutana," alisema.

"Wakati serikali ilipoamua kutumia force account tuliyumba sana na nilidhani tumejifunza kwa yaliyotokea wakati huo kwamba ungekuwa wakati mwafaka wa kukutana na kujadiliana namna ya kuwa na sauti moja, lakini naona bado," alisema.

Mratibu wa Mafunzo wa CRB, Msanifu Majengo Neema Fuime, alisema mafunzo hayo ya mara kwa mara yanalenga kuwapa makandarasi wa ndani uwezo wa kujaza zabuni kitaalamu wanapoomba kazi.

Alisema awali baadhi ya watoa kazi walikuwa wakilalamika kuwa makandarasi wengi hawana uwezo wa kujaza zabuni ndiyo sababu CRB ikachukua jukumu la kuwapa mafunzo hayo.



Naibu Msajili wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), David Jere, akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa makandarasi wazalendo mkoani Morogoro jana. Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi ya CRB, Consolata Ngimbwa na Makamu Mwenyekiti wa bodi hiyo, Joseph Tango. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Upimaji ardhi vijijini wamkuna waziri

**Na Munir Shemweta,**
SINGIDA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameridhishwa na kupongeza mradi wa upimaji mipaka ya Vijiji na makazi katika Wilaya ya Ikungi mkoani Singida.

Mradi huo unatekelezwa kwa pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN WOMEN), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) na Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Korea Kusini (KOICA).

Kupitia mradi huo unaotekelezwa kwa miaka mitatu hadi mwaka 2023, wananchi wa Ikungi watapata hatimiliki za kimila na utagharimu Dola za Marekani milioni 4.9. Unatarajia kuwafikia moja kwa moja wanawake na wasichana 2,350.

Akizungumza wakati wa kukagua mradi huo katika Kijiji cha Mnag'ana jana, Dk. Mabula alisema upimaji huo una faida kubwa kwa wananchi wa Ikungi kwa kuwa utawasaidia wanaopimiwa, kujua mipaka ya maeneo na kuepuka migogoro ya ardhi.

"Faida ya kupimiwa ni usalama wa miliki na uhakika wa kutambua maeneo hatimaye kuondokana na migogoro. Pia kutumia ardhi yako kwa kushughuli za maendeleo, kwa hiyo sasa serikali imefanya hivyo mara nyingi imekuwa ikiishia mijini na kusahau wale wa vijijini, wenye maeneo makubwa na sasa imeona itupie jicho maeneo ya vijijini kama Ikungi," alisema.

Aidha, Dk. Mabula alisema kupitia mradi huo wa UN WOMEN, mbali na kunufaisha vijana kupitia fedha wanazopata katika ushiriki wa kazi hiyo, pia unatoa fursa ya ujuzi kwa vijana kwa kupeleka katika maeneo mengine kile kilichofanyika katika Kijiji cha Mang'ana.

"Mradi huu unatumia teknolojia na taarifa zote zinaingia kwenye mfumo, hivyo hakuna mtu mwingine anaeweza kuingizwa katika kiwanja kimoja, hivyo takwimu ni faida ya mradi huo," alisema Dk. Mabula.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Singida, Shamim Hozza, aliuelezea mradi huo wa upimaji kama mradi wezeshi wenye lengo la kuwafanya wananchi maeneo yanayofanyiwa upimaji kushiriki katika upimaji.

"Mradi huu wa upimaji hapa Ikungi pamoja na kuwawezesha wananchi wanaopimiwa maeneo yao kuwa na hati za kimila, pia una lengo la kuwafanya wananchi kushiriki katika upimaji na kupatiwa hati za kimila," alisema Hozza.

## Kiongozi wa Mwenge ataka ushirikishwaji

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

KIONGOZI wa Mwenge wa Uhuru 2021, Luteni Josephine Mwambashi, amewaagiza wasimamizi wa miradi ya maendeleo kuwashirikisha wananchi kwa kila kinachofanyika.

Luteni Mwambashi alitoa maagizo hayo jana, wakati Mwenge wa Uhuru ulipokuwa ukipita na kukagua, kuweka mawe ya msingi kwa miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kuzindua.

Akiwa katika mradi wa kusambaza maji wa Mlandizi -Mboga unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salam (DAWASA), alisema ni lazima wananchi washirikishwe kwa kuwa ndio wanufaika.

Mwambashi alisema wanaohusika na kusimamia miradi hiyo ya maendeleo wanatakiwa kuhakikisha wanawapa wananchi taarifa za hatua mbalimbali za miradi hiyo na gharama zake.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema mradi huo unatarajiwa kukamilika Septemba, mwaka huu, kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 17, ambazo zinatolewa na serikali kuu.

Luhemeja alisema hadi sasa mradi huo umefikia asilimia 95 ya utekelezaji na fedha zilizotumika hadi sasa ni Sh. bilioni 13 na utakapokamilika utanufaisha wananchi 110,000.

Mwenge huo pia, ulizindua mradi wa Hoteli ya Msolwa inayomilikiwa na mwekezaji Jackson Mushi, ambao umegharimu zaidi ya Sh. bilioni moja hadi kukamilika.

Akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka Mkoa wa Morogoro, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema utakimbizwa katika Wilaya saba na miradi 87, yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 57, itazinduliwa.

HABARI KITAIFA

# TACAIDS yatakiwa kupambana na VVU kwenye miradi mikubwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeitaka Kamisheni ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini (TACAIDS), kuimarisha mapambano ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), kwenye miradi mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa ikiwamo mradi wa bomba la mafuta.

Pia, imetakiwa kudhibiti maambukizi mapya kwa kundi la vijana ambalo utafiti unaonyesha zaidi ya theluthi moja ya maambukizi hayo hutokea kwa vijana wenye umri wa miaka 15-28 hasa wa kike.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, aliyasema hayo jana alipokuwa akizindua kamisheni hiyo, jijini hapa.

Alisema maeneo ya miradi hiyo ya kimkakati ni hatarishi na yana mkusanyiko mkubwa wa watu na kwamba kuna haja kuweka mikakati.

"Tutaanza kutekeleza mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima kuja Tanzania, eneo hilo nalo ni hatarishi kwasababu lina mkusanyiko mkubwa, ujenzi wa SGR na maeneo kama hayo," alisema.

Akizungumzia maambukizi mapya, Mhagama alisema licha ya kuwapo na mafanikio mbalimbali kwenye mapambano ya ugonjwa huo, kuna haja ya kutokomeza maambukizi hayo.

"Ili kufikia malengo ya kidunia ya mwaka 2030 ya kuhakikisha tunakuwa na ziro UKIMWI kwenye mataifa yetu, kuna haja ya kuimarisha jitihada zetu katika kuzuia maambukizi mapya ya VVU hasa kwa vijana," alisema.

Alisema inawezekana kutokomeza maambukizi hayo kama ilivyofanikiwa kuzuia maambukizi ya VVU kwa mama kwenda kwa mtoto.

"Tumepata mafanikio ya kudhibiti maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto kutoka asilimia 18 hadi saba tuwapongeze wajawazito tumeokoa sana watoto maana wangezaliwa na maambukizi, kwa hiyo tunaweza hata kwenye kundi hili la vijana na ni ajenda muhimu sana," alisema.

Alisisitiza kuimarishwa kwa huduma za upimaji na matumizi ya dawa za kufubaza makali ya VVU (ARVs) kwa makundi maalum kwa jamii.

"Makundi maalum ni pamoja na watu wenye ulemavu, wavuvi ambao wanafanya kazi usiku na mchana, wale waliopo kwenye makundi hatarishi, madereva wa masafa marefu lazima kuwa na mkakati wa ziada kuhakikisha upimaji unafanyika, kwasababu hatuwezi matumizi mazuri ya ARV kama hatujafanikiwa kwenye upimaji," alisema. Alisema watu wanaojihusisha na biashara ya ngono wanatakiwa kuhamasishwa kupima afya zao na kujenga ushawishi wa kuwaondoa kwenye biashara hiyo.

Awali, Waziri Mhagama alisema takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kudhibiti ugonjwa wa Ukimwi na kiwango cha upimaji afya kwa Watanzania kimeongezeka kutoka asilimia 61 kwa mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 83 kwa mwaka 2019.

"Matumizi ya dawa za kufubaza VVU na Ukimwi kwa wanaoishi na VVU ambao wanajua hali zao za maambukizi yameongezeka kutoka asilimia 95 kwa mwaka 2016 hadi asilimia 98 hivi sasa, nakupongeza Mwenyekiti kwa kuwa uliongoza kamisheni hiyo," alisema.

Alisema vifo vinavyotokana na Ukimwi vimepungua kwa asilimia 50 kutoka 64,000 mwaka 2010 hadi kufikia 32,000 mwaka 2020.

"Maambukizi mapya kwa watu wazima yamepungua kutoka 110,000 hadi kufikia 68,000 kwa mwaka 2020, tunaona tunakwenda vizuri," alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Kamisheni hiyo, Dk. Hedwiga Swai, alihakikishia serikali kuwa watatimiza majukumu yao kwa weledi kwa kuzingatia sheria ili TACAIDS ifanye kazi kwa ufanisi.

Mkurugenzi wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alisema watafanya kazi na wajumbe wa Kamisheni hiyo ili kuhakikisha tatizo la Ukimwi linadhibitiwa.

## Walia corona kuporomosha bei ya tangawizi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAKULIMA wa tangawizi mkoani Kigoma wamepata hasara katika msimu wa mavuno wa zao hilo baada ya bei kushuka kutoka shilingi 1,000 na kuuzwa shilingi 300.

Baadhi ya wakulima kutoka Kata ya Kalela Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma, wamesema awali walitegemea zaidi kuuza katika soko la nje, lakini baada ya mlipuko wa ugonjwa wa corona imekuwa ngumu kulifikia soko hilo, kutokana na wafanyabiashara kutoka nchi hizo kushindwa kuja nchini kununua zao hilo. Masumbuko Ndemeye, alisema wanalazimika kuuzia madalali ambao ndio wamekuwa wakiwasiliana moja kwa moja na wafanyabiashara hao waliokuwa wakitoka za Rwanda, Burundi, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Malawi, japo anaamini inawezekana wamekuwa wakitumia mwanya huo kuwanyonya.

Alieleza wanalazimika kuuza kwa hasara kwa sababu hakuna soko lingine, hivyo kuomba serikali kusaidia kutengeneza mfumo wa masoko kama ilivyo katika mazao mengine ya biashara ili kumwezesha mkulima kujikwamua.

Melda Kisunzu, alisema amevuna tani moja ya tangawizi, lakini mauzo amepata Sh. 300,000, ambayo katika uvunaji pia alilazimika kuweka watu wa kumsaidia na kusafirisha kutoka shambani hadi kilipo kituo cha manunuzi.

"Kwa kweli nimepata hasara kubwa hata mtaji tu niliyotumia kukodi shamba na kuandaa haujarudi, serikali iliangalie jambo hili," alisema Kisunzu.

Ofisa Biashara Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma, Mushi Ndimuligo, alisema wakulima hao wanapaswa kuunda chama cha ushirika watakacho kuwa wanakusanyia zao hilo na kutafuta masoko kwa pamoja ikiwamo kusimamia bei.




Mkuu wa Maduka na Bidhaa za Tigo, Mkumbo Myonga, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati Tigo kwa kushirikiana na kampuni ya Sanlam, walipozindua huduma ya bima ya simu janja, kwa ajili ya simu zinazopotea, kuharibika kwa bahati mbaya au kuibiwa. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa Sanlam, Geoffrey Masige. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tigo, Sanlam wazindua bima ya simu za mkononi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kidijitali ya Tigo Tanzania, imeshirikiana na kampuni ya Sanlam, kuanzisha bima ya simu janja (Smartphones).

Imeelezwa kuwa huduma hii ni kwa simu mpya zinazonunuliwa katika maduka ya Tigo nchini kote. Mpango huu ni kwa ajili ya simu zinazopotea, kuharibika kwa bahati mbaya au kuibiwa.

Akizungumzia ushirikiano huo, Mkuu wa Maduka na Bidhaa za Tigo, Mkumbo Myonga, alisema, katika ulimwengu ambapo simu janja zimekuwa muhimu sana kwa watu wengi ambao huzitegemea kuwasiliana na dunia kupitia mitandao ya kijamii, huku wengine wakizitumia kama ofisi zao za kazi.

Alisema ushirikiano huu na Sanlam utawapa bima wamiliki wa simu za mkononi endapo simu zao zitapotea au kuharibika.

"Baada ya wateja kununua simu kutoka kwenye maduka yetu, mbali na dhamana ya kawaida, tunashauri wakatie bima simu janja zao mpya. Mpango huu unakidhi haja za wateja wetu, hususani wanaotaka kulinda simu zao zinazoharibika au kupasuka kwa bahati mbaya. Muda wa bima utakuwa ni miezi 12 ambapo mmiliki wa simu atatakiwa kulipa asilimia 5 ya jumla ya gharama ya kununulia simu yake ya mkononi kama malipo ya bima," alieleza Mkumbo.

Wateja wanaweza kupata bima ya simu janja kwa kutembelea maduka ya Tigo yaliyopo nchi nzima."

Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa Sanlam, Geofray Masige, alisema, mpango huu wa bima, utahakikisha kuwa wateja wa Tigo wanatengenezewa au kurudishiwa simu zao haraka baada ya kuharibika au kupotea ndani ya muda uliowekwa.

"Simu janja sasa imekuwa ni sehemu ya maisha ya kila siku ya wanadamu. Ukiachia mbali gharama halisi ya kununulia, kifaa hiki kina thamani kubwa kwa mtumiaji wake na hofu ya kupoteza ni kubwa kwa watu wengi, lakini kwa hili Sanlam na Tigo tumeleta suluhisho," alisema.

Masige aliongeza kuwa, mpango wa bima ya simu za mkononi ni nafuu sana na kujiandikisha ni rahisi sana, maana hakuna kutumia makaratasi, bali taarifa zote za mteja zitahifadhiwa kidijitali.

# Wenye ulemavu walalamikia Sheria ya Usalama Barabarani

**Na Thobias Mwanakatwe**

WATU wenye ulemavu wameitaka serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Usalama Barabarani, kwa kuwa iliyopo haiwajali watumiaji wa barabara ambao ni wenye ulemavu.

Wamesema hali hiyo inasababisha kuongezeka kwa ulemavu nchini na wengi kupoteza maisha kutokana na ajali.

Hayo yamebainishwa na mawakili wabobezi na Vyama vya Watu wenye Ulemavu kwenye kikao kazi cha kuchambua Sheria ya Usalama Barabarani namba 168 ya mwaka 1973, ambacho kiliandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Ofisa Programu LHRC, Joramu Bwire, alisema lengo la kuipitia sheria hiyo na kanuni zake ni kwa sababu haiweki bayana ulinzi kwa watu wenye ulemavu ambao nao ni watumiaji wa barabara na hivyo kusababisha wapate ajali mara kwa mara.

Naye Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Jonas Lubago, alisema Sheria ya Usalama Barabarani ipo kimya juu ya watumiaji barabara wenye ulemavu wa aina mbalimbali, hali inayosababisha changamoto na kuleta madhara mengi na hata kupoteza maisha.

"Watu wenye ulemavu wengi wamekuwa wakigongwa kutokana na madereva kutojua jinsi ya kutoa ushirikiano kwa watumiaji wa barabara wenye ulemavu," alisema.

Lubago alisema sheria hiyo haitoi mkazo mahususi kwa kuzienzeza alama za barabarani za watu wenye ulemavu na pia alama hizo hazitambuliki na sheria na hakuna hata dereva mmoja aliyewahi kufundishwa kwenye vyuo vya udereva. Aliongeza kuwa hata alama za barabarani za wenye ulemavu zilizopo, serikali kupitia mamlaka husika haijazisimika kwenye maeneo yanayohitajika hali ambayo inasababisha ajali nyingi zinazohusisha wenye ulemavu.

"Sheria ya Usalama Barabarani inatakiwa kuzungumza kwa upana juu ya haki za watu wenye ulemavu wawapo barabarani na kwenye vyombo vya usafiri kama zinavyobainishwa katika Sheria ya Watu wenye Ulemavu Namba 9 ya 2010, Sera ya Watu wenye Ulemavu ya 2004 na mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu ya mwaka 2006," alisema.

Mwendo katika korido na nafasi kati ya kiti na kiti inayoruhusu mtu mwenye ulemavu kuketi.

Mshiriki wa kikao hicho, Pepetua Senkolo, alisema kufanyika kwa kikao hiki na mapendekezo yatakayotolewa yatasaidia kuboresho marekebisho ya sheria ya barabarani ili iwe rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Mapendekezo yatakayotolewa kwenye kikao hicho yatawasilishwa serikalini ili serikali ione jinsi ya kuingiza hoja zinazolinda haki ya mtu mwenye ulemavu katika matumizi ya barabara.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Tanzania Tamil Sangam, Balasubramaniyan Venkadachalam (kushoto) na Ofisa Elimu ya Msingi wa Jiji la Dar es Salaam, Sipora Tenga (wapili kushoto), wakikabidhi madawati 37 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 4.8 kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Upanga, Airika Yahaya (wapili kulia), yaliyotolewa msaada na taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Zanaki, Adolph Rwegoshora (watatu kushoto) na Karthikeyan Palanisamy wa wa taasisi hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizi waibuka miche iliyofanyiwa utafiti

**Na Ashton Balaigwa,** KIGOMA

KUMEIBUKA wizi wa miche bora ya michikichi aina ya Tenera katika mashamba ya taasisi za serikali na zisizo za kiserikali na kutoa ishara ya kuwapo kwa mahitaji makubwa ya miche hiyo iliyofanyiwa utafiti na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI).

Miongoni mwa taasisi za serikali zinazoendesha kilimo hicho zilizokumbwa na wizi huo ni shule za msingi na sekondari na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Msalaba Mwekundu (Red Cross).

Wizi huo umetajwa kwenye halmashauri za Wilaya ya Kasulu, Mji wa Kasulu na Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Imanga iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Carlos Mabula, alisema jana kuwa baada ya kupewa miche hiyo na TARI, walipanda katika shamba lao lakini baada ya siku mbili iliibwa.

Msimamizi wa Shamba la Msalaba Mwekundu, Yubert Bihali, kutoka Kijiji cha Kanazi, Halmashauri ya Kasulu Mji, alisema walipanda miche ya michikichi aina ya tenera 1,196 katika shamba lao lenye ukubwa wa ekari 23, lakini baadhi ilibwa na wanakijiji na katika kufuatilia walibaini wakulima waliienda kupanda katika mashamba yao.

"Hii miche ya michikichi aina ya tenera ilitolewa bure na Wizara ya Kilimo mwaka jana na tukapanda.

"Wapo waliokuwa na dhana potofu kuhusu miche hii, baada ya kuona ina ubora na inaweza kuzalisha kwa muda mfupi, hivi sasa baadhi yao wameingia katika shamba letu na kung'oa na kwenda kupanda katika mashamba yao.

"Tunaomba serikali iongeze uzalishaji, inaonekana kuna mwamko mkubwa wa kilimo hiki," alisema Bihali.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kitongoni iliyoko Manispaa ya Kigoma Ujiji, Ismail Kibalo, alisema walipewa miche hiyo ya michikichi na kuipanda katika shamba la shule hiyo ikiwa ni mwitikio wa agizo la Waziri Mkuu, Majaliwa Kassim, kupanda zao hilo.

Hata hivyo, miche hiyo iliibwa katika shamba hilo na mingine kuliwa na mifugo.

Mkuu wa Idara ya Kilimo Manispaa ya Kigoma Ujiji, Evance Mdee, alisema hicho ni kiashiria cha kuwapo kwa mahitaji makubwa ya miche hiyo bora, hivyo kwa kushirikiana na TARI wanajipanga kuzalisha miche mingine ya michikichi aina ya tenera ili kuigawa bure kwa wakulima na taasisi zote zenye mahitaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Joseph Kashushura, alisema kutokana na kuwapo kwa mahitaji ya miche kwa wakulima, halmashauri hiyo imeamua kutenga fedha kwa ajili ya kuzalisha miche mingi zaidi ili kuigawa bure kwa wakulima.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema taasisi hiyo kupitia Wizara ya Kilimo imekuwa ikizalisha miche bora ya kisasa aina ya tenera na kugawa bure ili kuendeleza kilimo bora cha michikichi na kuliwezesha taifa kujitegemea katika kuzalisha mafuta ya kula.

Dk. Mkamilo alionya kuwa mbegu hiyo ina gharama kubwa na serikali haitamvumilia mtu yeyote anayefanya uharibifu wa miche hiyo ikiwa pamoja na kuingiza mifugo kwenye mashamba ya michikichi.

## THDRC yafunguka kukosa watetezi

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Nchini (THDRC), umeomba mashirika na watu binafsi kujiunga nao ili kuendelea kutetea haki za watu wa makundi mbalimbali.

Ombi hilo lilitolewa jana jijini Mwanza na Mratibu Taifa wa mtandao huo, Onesmo Olengurumwa, alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema moja ya vikwazo wanavyokumbana navyo kama shirika, ni kukosa watetezi wa makundi ya walemavu, ufuatiliaji na uwajibikaji.

"Kuna maeneo ya haki za binadamu hayapati watetezi kama ilivyo kwa watoto na wanawake wengi wamekuwa wakijikita katika masuala ya huduma za afya, elimu na mashirika yanayofanya katika maeneo haya ni yale ya kimataifa," alisema Olengurumwa.

Alisema yapo maeneo ambayo yanahitaji kushughulikiwa zaidi kutetea haki ambayo hayajaguswa mpaka sasa.

Olengurumwa alisema rasilimali zimekuwa kikwazo kwao jambo ambalo limesababisha kukosa fedha za kuendeshea miradi.

"Miradi mingi inayoanzishwa ni ya muda mfupi, mfano miezi mitatu, hii inafanya usiwe na uhakika wa raslimali kwani mingine inatokana na mashirika ya kimataifa yanakuja na kuingia ubia," alisema Olengurumwa.

Alitaja sababu nyingine ni pamoja na fedha za kusaidia mashirika yanayotetea haki za binadamu ni ugonjwa wa corona ambao umechangia wafadhili kuondoka nchini.

Aidha, alisema wanachama wao wamekumbwa na tatizo la kuondokewa na wafadhili na hivyo kukosa fedha za kuendeshea miradi, ofisi na kuajiri watu.

Aliomba wafadhili kujitokeza kwa wingi katika kusaidia wanachama wao kufanikisha masuala ya utetezi wa haki za binadamu katika makundi mbalimbali.

Kwa upande wake, mwanachama wa THDRC, Jimmy Luhende, alisema hawajapata wanachama wa kutosha kushirikiana nao katika kutetea haki za binadamu.

Alisema wanafanya kazi ya kuwasaidia wananchi ili kupunguza hofu na kuwa na uwezo wa kuhoji.

"Tunafanya kazi ya kuwasaidia wananchi kupunguza hofu, wawe na uwezo wa kuhoji kama vile watu wanaofanya kazi migodini na wakulima wadogo," alisema Luhende.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Chama cha Wafanyakazi wa Tasnia ya Nishati na Madini, aliomba miundombinu ya utoaji wa haki katika maeneo mbalimbali kuboreshwa.

# ama

AFYA NA MAZINGIRA

ALHAMISI AGOSTI 12, 2021



Ukurasa 14

**Kampeni za TB zaja kivingine, sasa ni nyumba kwa nyumba**



Ukurasa 13

Ndege Ulaya na sitatunga wanavyoing'arisha Rubondo



Ukurasa 12

**EATV, East Africa Radio wanavyochanja mbuga kwenye kampeni ya 'Namthamini'**

# Dunia sasa inaelekea ukingoni sababu ni mabadiliko tabianchi

**Na Christina Mwakangale**

• Bahari kuchemka, theluji milimani 'kwishinei'

HALI ya ongezeko la joto duniani, inayoripotiwa na Jopo la Umoja wa Mataifa la Wanamazingira wa Mataifa Mbalimbali (IPCC), inaonyesha kuwa kiama cha binadamu hakiko mbali, ni kwa vile inaasharia hatari kwa sayari hiyo pamoja na viumbe wake.

Chanzo kikuu ni shughuli za binadamu zinazobadili hali ya hewa kwa njia zisizotarajiwa na wakati mwingine zisizoweza kurekebishwa, utafiti wa kihistoria unaonya kuhusu kuongezeka kwa joto kali, ukame, mafuriko na kuvukwa kwa ukomo wa joto duniani katika kipindi cha muongo mmoja ujao, yaani ifikapo 2030.

Ripoti hiyo ya IPCC inayofanyakazi na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCC), inatoa ishara ya hatari kwa binadamu', anasema Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Wanasayansi wanasema janga hilo linaweza kuepukika, iwapo dunia itachukua hatua za haraka, na kwamba wana matumaini kuwa kupunguzwa kwa kiwango kikubwa zaidi cha utoaji wa hewa ukaa kutasaidia kuzuia kuongezeka zaidi kwa viwango vya joto duniani.

Akiunga mkono matokeo ya utafiti ya wanasayansi, Katibu Mkuu wa UN António Guterres anasema: "Iwapo tutaweka pamoja nguvu, tunaweza kuepuka janga la hali ya mabadiliko ya hali ya hewa duniani".

"Lakini hadi leo, ripoti inabainisha wazi kuwa hakuna muda wa kuchelewa na hakuna muda wa kutoa sababu. Ninawategemea viongozi wa serikali na wadau wote kuhakikisha mafanikio ya Mkutano wa Dunia wa Jinsi ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa Copenhagen 26 (COP26) yanafikiwa."



Moto wa asili unaoendelea nchini Uturuki ni moja ya majanga yanayotokana na uharibifu uliokithiri wa mazingira duniani. **PICHA: MTANDAO**

**IPCC YAONYA NI KITISHO**

Tathmini ya hali ya hewa ya dunia imefanywa na jopo la Umoja wa Mataifa la Wanamazingira wa Mataifa mbalimbali IPCC na kikundi cha wanasayansi ambao kazi yao iliidhinishwa na serikali za dunia. Jopo hilo linaloongoza ripoti, ambazo zitachapishwa kwa miezi kadhaa ijayo ni tathmini kuu ya kwanza ya sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa duniani kuwahi kufanyika tangu mwaka 2013.

Waraka wa IPCC unasema, bila shaka ushawishi wa binadamu umechemsha anga, bahari na ardhi na kwamba matendo yake yamesababisha mabadiliko ya tabianchi na kufanya dunia kuwa na joto zaidi.

Profesa Ed Hawkins kutoka Chuo Kikuu cha Reading, Uingereza, ambaye pia ni mmoja wa waandishi wa ripoti hiyo, anasema wanasayansi hawawezi kuwa wazi zaidi ya hali ilivyo kwa sasa.

Waandishi wa ripoti wanasema kwamba tangu mwaka 1970, viwango vya joto kwenye sakafu ya dunia vimeongezeka haraka zaidi, kuliko ilivyowahi kutokea katika mwaka wa 50, kwa miaka 200 iliyopita.

Moto wa asili unaoshuhudiwa Ugiriki na Marekani Magharibi, mafuriko kama yale yaliyotokea Ujerumani na China ni kielelezo kuwa shughuli za binadamu zimechangia kwa zaidi ya muongo mmoja uliopita kuchemsha na kuchochoa kasi ya mabadiliko ya tabianchi.

**YALIYOBAINISHWA NA IPCC**

Ripoti hiyo pia inabainisha wazi kuwa joto linalolishuhudia leo limesababisha mabadiliko kwa mifumo mingi ya sayari, athari ambazo haziwezi kurekebishika kwa kipindi cha karne (miaka 100) hadi milenia (miaka 1,000) kutokana na jinsi uharibifu ulivyokuwa mkubwa

Ripoti inasema bahari zitaendelea kuchemka na kuwa na tindikali zaidi na barafu za vilele vya milima zitaendelea kuyeyuka kwa miongo au karne kutokana na joto na kwamba athari zitaendelea kuwa mbaya zaidi kila mara dunia inapochemka , anasema Profesa Hawkins.

Jimbo la California linalokabiliwa na ukame limeshuhudia kupungua kwa viwango vya maji katika ziwa Oroville, lakini linapokuja suala la kupanda kwa viwango vya maji ya bahari, wanasayansi wameelezea kuwa uwezekano wa ongezeko la viwango tofauti vya maji umesababishwa na utoaji wa hewa chafu.

Hata hivyo, ongezeko la karibu mita mbili kimo cha maji mwishoni mwa karne hii haliwezi kupuuzwa na ongezeko la mita

INAENDELEA UK.13

AFYA

# EATV, East Africa Radio wanavyochanja mbuga kwenye kampeni ya 'Namthamini'

- Kwa miaka minne wafika zaidi ya mikoa 15
- Wasichana kibao wasaidiwa taulo za kike

**Na Sabato Kasika**

UPATIKANAJI wa taulo za kike, ni moja ya mambo yanayotiliwa mkazo na wadau mbalimbali, ili kusaidia wasichana wanaosoma msingi na sekondari kuwa na hedhi salama katika mazingira yoyote, ili hali hiyo ya kimaumbile isiwakwamishe kuendelea kitaaluma.

Vituo vya EATV na East Africa Radio ambavyo ni sehemu ya Kampuni za IPP, ni miongoni mwa wadau ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakifanya kampeni za kuwezesha upatikanaji wa taulo za kutosha kwa ajili ya kundi hilo.

Tangu mwaka 2017 kwa kutumia kampeni yao ya 'Namthamini', wamefanikiwa kufika zaidi ya mikoa 15 baadhi yake ikiwa ni Dodoma, Mbeya na Mwanza na kugawa taulo hizo kwa wasichana zaidi ya 11,000.

Mratibu wa kampeni hizo za 'Namthamini', Sophia Mng'anya, anaitaja mikoa mingine kuwa ni Dar es Salaam, Arusha, Pwani, Mara, Kigoma, Manyara, Tabora, Morogoro na Njombe.

"Wanafunzi wa kike hukosa wastani wa jumla ya siku 60 za masomo kwa mwaka wanapokuwa katika hedhi, kutokana na kukosa taulo za kike za kujisitiri," anasema Sophia.

Anasema, hali hiyo ndiyo iliwasukuma kuanzisha kampeni ya 'Namthamini' kupitia vituo vya EATV na East Africa Radio na kufanikiwa kufikia zaidi ya mikoa 15 huku wasichana zaidi ya 11,000 wakisaidiwa taulo hizo.

"Takwimu mbalimbali zilionyesha kuwa wanafunzi wa kike walio katika mazingira magumu, hukosa masomo kwa muda wa siku tano hadi saba kwa mwezi, hivyo kuna haja ya kuwasaidia kupata taulo," anasema.




Mkurugenzi Mtendaji wa EATV na East Africa Radio, Regina Mengi (kushoto) na Flaviana Matata baada ya kusaini mkataba wa ushirikiano. **NA MPIGAPICHA WETU**

### USHIRIKIANO WA WADAU

Katika mwendelezo wa kampeni hizo, anasema, vituo vya EATV na East Africa Radio vimeanza ngwe nyingine ya kumsaidia mtoto wa kike kwenye suala la hedhi salama kwa kushirikiana na wadau wengine.

"Tumeingia mkataba wa ushirikiano na Tasisi ya Flaviana Matata Foundation, ili kusaidiana katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuchaangia chochote, kwa ajili ya upatikanaji wa taulo za kike," anasema.

Anasema, mkataba huo wa mwaka mmoja, umesainiwa hivi karibuni kati ya Mkurugenzi Mtendaji wa EATV na East Africa Radio, Regina Mengi na mwanzilishi wa Taasisi ya Flaviana Matata Foundation, Flaviana Matata.

> **Watu wanaweza kuchangia fedha kupitia akaunti namba 01504319 38200 benki ya CRDB, jina ni NAMTHAMINI.**

Akizungumzia mkataba huo, Sophia anawaomba Watanzania kushirikiana na vituo hivyo katika kampeni hiyo kwa kuchangia taulo za kike au fedha, ili kumsaidia mtoto wa kike kupata elimu bila vikwazo.

Mratibu huyo anasema, mtoto wa kike ana ndoto zake katika maisha kama alivyo wa kiume, hivyo ili ziweze kutimia, ni muhimu asaidiwe kwa ajili ya kuhakikisha hedhi siyo kikwazo kufikia malengo aliojiwekea.

"Watu wanaweza kuchangia fedha kupitia akaunti namba 0150431938200 benki ya CRDB, jina ni NAMTHAMINI, au kutuma fedha kupitia namba ya malipo ya Selcom Mastercard 6057 9851," anasema.

Mbali na kutumia njia hiyo, anasema mdau anaweza kuwasilisha mchango wake wa taulo za kike pedi au fedha katika ofisi za East Africa Television na East Africa Radio Mikocheni Dar es Salaam, vyote wanavipokea.

Sophia anasema, mtoto wa kike anapoinuliwa ni sawa na kuinua jamii nzima, na kwamba wao EATV na East Africa Radio wameacha milango wazi kwa Watanzania kuunga mkono kampeni za 'Namthamini'.

Anafafanua kuwa kampeni hiyo inaendeshwa kwa kuchangia pesa taslimu, ambazo zitatumika kununua taulo za kike, pia wanapokea taulo hizo na kuhakikisha zinawafikia walengwa kwa muda muafaka.

Mkurugenzi wa taasisi iliyoingia mkataba wa ushirikiano na vituo hivyo, Flaviana Matata, anasema anashukuru kuungana na wadau wenzake katika harakati za kumwezesha mtoto wa kike kupata hedhi salama.

"Kwa muda mrefu tumekuwa tukiendesha kampeni za kugawa taulo za kike, hivyo kuungana na wadau wenzetu katika kampeni hizi kuelimisha umma kuhusu hedhi salama ni jambo la muhimu," anasema Flaviana.

### HEDHI NI MAUMBILE

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto, Dk. Dorothy Gwajima, anasema hedhi si ugonjwa wala laana bali ni uumbaji wa Mungu katika kumkamilisha mwanamke.

Hata hivyo, waziri huyo anasema, baadhi ya wasichana na wanawake, wanakuwa katika mazingira ya kutokua na hedhi salama kutokana na miundombinu duni ya vyoo.

"Kukosekana kwa maji safi na salama, matumizi ya vifaa vya hedhi visivyo salama na utupaji ovyo wa vifaa vilivyotumika, huchangia kuwapo kwa hedhi isiyo salama kwa baadhi ya wasichana na wanawake," anasema Dk. Gwajima.

Anasema matokeo ya utafiti uliofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMRI) na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na wadau wa hedhi salama mwaka 2019, ulionyesha nchi imepiga hatua kubwa.

"Hatua hiyo ni maendeleo ya ajenda ya afya ya hedhi salama, ingawa bado kuna changamoto katika ngazi ya jamii kutokana na uelewa mdogo wa hedhi salama. Asilimia 28 ya wasichana ndio wanaoelewa hedhi salama," anasema.

Anataja baadhi ya Halmashauri ambazo baadhi ya watu wake hawana uelewa juu ya hedhi salama kuwa ni Namtumbo mkoani Ruvuma, Mbeya, Muleba mkoani Kagera, Temeke Dar es Salaam na Igunga mkoani Tabora.

Halmashauri nyingine zilizofanyiwa utafiti na kugundua hali hiyo anazitaja kuwa ni Karatu mkoani Arusha, Tandahimba mkoani Mtwara, Rorya mkoani Mara, Kusini Unguja na Kaskazini Pemba.

Anaongeza kuwa utafiti huo wa NIMR, ulionyesha kuwa asilimia 60 ya wasichana walionekana kutomudu za taulo za kike, hali anabainisha kuwa uhamasishaji wa kupata taulo hizo unahitajika zaidi.

"Ninawashukuru wadau wote kwa kuendelea kuhamasisha upatikanaji wa vifaa vya hedhi salama ndani ya nchi yetu, kwa unafuu na ubora unaotakiwa, ili kila mhitaji kwa makundi yote aweze kutumia," anasema Waziri.

MAZINGIRA



Ndege Ulaya na sitatunga vivutio mujarabu vya Hifadhi ya Rubondo. **PICHA: MTANDAO**

# Ndege Ulaya na sitatunga wanavyoing'arisha Rubondo

**Na Alphonce Kabilondo,**
CHATO

NDEGE wanaosafiri kutoka Bara la Ulaya ni mojawapo ya vichocheo vikubwa kwa watalii wanaozuru kisiwa cha Rubondo Wilaya ya Chato mkoani Geita.

Maajabu hayo yasingekuwapo kama juhudi za kutunza mazingira na kuhifadhi maeneo ya asili na mazalia ya wanyama , wadudu na ndege, kama misitu, maji, ardhi oevu na mimea zisingesimamiwa kikamilifu.

Katika hifadhi hiyo kuna eneo la Irumo lililokuwa likitumiwa na wenyeji Wazinza kama sehemu ya matambiko na kujiondolea na mikosi, ambalo lina kina kirefu zaidi cha mita 80 kwenda chini ya ardhi katika Ziwa Victoria na kuna mwamba ndani yake.

Ndege wanaodaiwa kusafiri kutoka Bara la Ulaya hadi kisiwa hicho wanaotumia dagaa kama kitoweo chao . Joshua Deo ni mmoja wa watalii mwenye asili ya Uingereza aliyekutana na gazeti hili kwenye hifadhi hiyo, anasema kuwa amenza kufanya utalii kwenye hifadhi hiyo tangu akiwa mtoto akiletwa na wazazi wake .

"Hakuna hifadhi nzuri kama hifadhi ya kisiwa cha Rubondo, ina vivutio vingi msitu wa asili na wanyama adhimu kwa wakati wote . Imekuwa hivi kwa sababu ya kutunza mazingira na kuendeleza uhifadhi," anasema.

Ofisa Utalii Bodi ya Utalii, Naomi Mbilinyi anabainisha haya , "upekee wa hifadhi ya kisiwa hicho ni kuwa na ndege wa ajabu wanaodaiwa kusafiri kutoka Ulaya hadi kisiwa cha Rubondo wanaoshawishi watu na watalii mbalimbali kuja kuwaangalia."

Anamtaja mnyama aina ya nzohe au sitatunga anayepatikana katika hifadhi hiyo pekee na maeneo mengine huko Nairobi Kenya.

"Utalii unaanza na Watanzania wenyewe, ndege hao waajabu wenye sauti za kuvutia pamoja na nzohe ni kichocheo kikubwa cha watalii katika hifadhi hiyo, hivyo ni vyema tuwe na utamaduni wa kufanya utalii wa ndani na kutunza mazingira yetu,"anasema Ofisa Utalii Naomi.

Hifadhi ya Taifa ya Rubondo iliyopo katika Wilaya ya Chato ni moja kati hifadhi za taifa katika ukanda wa magharibi zinazo simamiwa na Shirika la Utalii Nchini (TANAPA).

> **Kisiwa cha Rubondo ni kitovu cha ziwa Victoria kutokana na samaki wake kusambaa katika ziwa hilo .**

Sekta ya utalii nchini inachangia pato la taifa kwa asilimia 17, wakati inachangia asilimia 25 ya fedha kigeni kutokana na watalii wa ndani na nje wanaotembelea hifadhi za taifa 22, zinazo simamiwa na TANAPA.

Aidha, pamoja na kuchangia pato la taifa na fedha za kigeni ni eneo linalotoa ajira kwa watu zaidi ya milioni 5.5 kwa mwaka, zikiwamo za kudumu na za muda msimu.

Miongoni mwao wapo waongoza watalii, wauza bidhaa mbalimbali, wahudumu mahotelini, migahawani, madereva na wajasiriamali wa sekta mbalimbali wanaonufaika na ujio wa wageni hao.

Akizungumzia ukubwa anasema hifadhi hiyo ina ukubwa wa kilometa za mraba 456.8 eneo la maji, nchi kavu lenye kilometa 236.8 na sehemu ya mazalia ya samaki ya kilometa za mraba 220.

Anasema kisiwa cha Rubondo ni kitovu cha ziwa Victoria kutokana na samaki wake kusambaa katika ziwa hilo .

## CORONA YAPUNGUZA WATALII

Mhifadhi wa Idara ya Utalii katika hifadhi ya kisiwa hicho, Themistocles Bitta, katika mahojiano na Nipashe anakiri kuwa idadi ya watalii wanaofika kutembelea hifadhi hiyo imepungua kutoka 2,000 na kufikia 1,500 baada ya janga la COVID-19 kuingia duniani.

Anazitaja aina za utalii katika kisiwa hicho ni ule wa kutembea kwa miguu, wa majini pamoja na wa kuvua samaki (sport fishing ) .

"Awali watu wengi walikuwa hawana elimu walikuwa wakidhani kuwa utalii mpaka raia wakigeni, sasa wametambua kuwa upo utalii wa ndani," anasema mhifadhi huyo .

Aidha, anaongeza kuwa vivutio vinavyo patikana katika hifadhi hiyo ni pamoja na samaki, mamba, twiga ,tembo, pongo, sokwe, kobe pamoja na msitu mnene wa asili na asilimia 80 pamoja na ndege .

Marth Mkumpasi ni Mkuu wa Wilaya ya Chato anasema kuwa, Wilaya hiyo kwa kushirikiana na hifadhi ya Kisiwa cha Rubondo wameanza kutoa elimu ya utalii na kuhamasisha utalii katika hifadhi za Ukanda wa Magharibi ikiwemo hifadhi hiyo na ya Burigi Chato .

"Chato tunazo hifadhi mbili Rubondo na Burigi, lakini tangu kuzinduliwa kwa hifadhi ya Burigi mwaka juzi, hakuna mwamko wa wananchi kwenda kufanya utalii wa ndani hivyo tumeanza kutoa elimu kupitia tamasha la utalii," anasema Mkuu wa Wilaya Mkumpasi.

# Dunia sasa inaelekea ukingoni sababu ni mabadiliko tabianchi

**INATOKA UK.11**

tano linaweza kuwapo kufikia mwaka 2050, ikielezwa kuwa ni matokeo ya aina hiyo ambayo huenda yasiwe kitisho kwa dunia, yanayoweza kutishia maisha ya mamilioni zaidi ya watu wanaoishi maeneo ya mwambao pamoja na mafurika ifikiapo mwaka 2100.

Wanchi wakiwamo waandamanaji wanataka viongozi kuchukua hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, takriban kila taifa duniani lilisaini malengo ya makubaliano ya Paris kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa mwaka 2015. Makubaliano yalilenga kuendelea kuviweka viwango vya joto la dunia chini ya nyuzi joto 2.0 na kujaribu kufanya juhudi za kuiweka chini ya nyuzi joto 1.5.

Athari za kwenda zaidi ya nyuzi joto 1.5 kwa kipindi cha miaka kadhaa ni kitu ambacho hakitapendwa katika dunia ambayo tayari imekwisha shuhudia matukio mabaya ya majanga huku viwango vya joto vikiongezeka tangu kabla ya enzi ya viwanda kwa kiwango cha nyuzijoto 1.1, anasema Profesa Hawkins.

## ATHARI ZINAZOTARAJIWA

Viwango vya joto vitafikia nyuzi joto 1.5 juu ya vile vya kati ya 1,850-1,900 ifikapo mwaka 2040 kwa kuzingatia aina zote za uchafuzi wa hali ya hewa, bahari ya Arctic itakuwa na uwezekano wa kutokuwa na barafu ifikapo mwezi Septemba, walau mara moja kabla ya 2050.

Pia kutakuwa na ongezeko la matukio mabaya zaidi yasiyotarajiwa katika rekodi ya historia hata katika nyuzi joto 1.5.

Pia, matukio ya kuongezeka kwa viwango vya juu, zaidi vya maji ambavyo hutokea mara moja kwa karne katika siku chache zilizopita yanakadiriwa kutokea walau kila mwaka kufikia mwaka 2100, anasema Dk. Otto,

Kadhalika kutakuwa na uwezekano wa kuongezeka kwa hewa ya moto katika maeneo mengi, huku makadirio yakionyesha ongezeko la viwango vya joto zaidi kuliko wakati wowote ule katika ripoti hiyo na athari nyingi haziwezi kuepukika, waandishi wa ripoti wametahadharisha dhidi ya athari hizo kusababisha vifo, anaongeza Dk Otto. **MTANDAO**

AFYA

# Kampeni za TB zaja kivingine, sasa ni nyumba kwa nyumba

**Na Mary Geofrey**

## • Wagonjwa kufuatwa, kupimwa na kufuatiliwa

TANZANIA inatajwa kuwa ni miongoni mwa nchi saba kinara barani Afrika zinazofanya vizuri katika mapambano dhidi ya Kifua Kikuu (TB) na baadhi ya mikakati yake sasa inaigwa na mataifa mengine.

Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara ya Afya Idara ya Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP) Dk. Zuwena Kondo, ananukuliwa akisema Tanzania imefanikiwa kutokana na kuimarishwa kwa upatakanaji wa takwimu za wagonjwa kwa kutumia wataalamu wa ndani, hivyo kuwezesha uendelevu wa mfumo huo na mafanikio ya kukabili maradhi hayo.

Nchi nyingine zinazotajwa kukabiliana na ugonjwa huo kikamilifu ni Kenya, Afrika Kusini, Burkina Faso, Nigeria na Msumbiji.

Dokta Zuwena anasema, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI TB na Malaria umetambua mfumo wa ufuatiliaji na kukusanya takwimu za wagonjwa unaoitwa 'DHIS2TL - Tracker Module ' ndiyo unaofanikisha na kwamba ni wa kwanza kufanikiwa katika nchi za Afrika ni bora na wa kuigwa.




Vifaa, zikiwamo baiskeli na vibeba sampuli za makohozi kwa watoa huduma kwa wenye TB majumbani. **PICHA: MARY GEOFREY**

### KUFIKIA WAGONJWA NYUMBANI

Shirika la kimataifa la Amref Health Africa nchini, kupitia mradi wake wa USAID Afya Shirikishi, unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) linatoa baiskeli 710 na vikasha 859 vya kubebea sampuli za makohozi, ili kufanyiwa vipimo vya TB, kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkazi wa Amref Health Africa Tanzania, Dk. Florence Temu.

Anasema vitendea kazi hivyo vinatolewa kwa ajili ya watumishi wa Afya (CHWs) walio katika mikoa ya Dar es Salaam, Geita, Katavi, Kigoma, Mwanza, Pwani, Rukwa, na Songwe, ili kuwafikia wagonjwa wa majumbani.

Mradi huo wa USAID Afya Shirikishi utatekelezwa kwa miaka mitano kuanzia 2021/25 na unalenga kuongeza na kuimarisha upatikanaji wa huduma za TB na afya ya uzazi katika ngazi ya jamii, anaongeza.

Mradi unakazia kupunguza maambukizi na kuendelea kwa Kifua Kikuu kupitia uimarishaji wa utoaji huduma katika ngazi ya jamii, kuimarisha upatikanaji

> **Kupitia Wizara ya Afya, tunashukuru sana kwa baiskeli hizi na makasha ya kukusanyia sampuli za makohozi ya TB, ambavyo vitatumika katika mikoa inayotekeleza mradi huu nchini.**

na matumizi ya huduma bora za uzazi wa mpango, kuimarisha uwazi, utoaji mrejesho, na upatikanaji wa takwimu zinazohusiana na programu za Kifua Kikuu.

Dokta Florence anasema lengo lingine ni kuimarisha sera na miongozo ya taifa ya TB na kuongeza uongozi na uungaji mkono wa kisiasa katika vita hiyo kama kipaumbele cha jamii.

Mradi huo wa miaka mitano unatekelezwa pia, kwa kushirikiana na Kituo cha Mawasiliano na Maendeleo cha Tanzania (TCDC), wadau wengine ni Mwitikio wa Kuthibiti Kifua Kikuu na UKIMWI Tanzania (MKUTA) na Huduma za Afya na Maendeleo kwa Watu Wanaoishi na VVU/ UKIMWI (SHDEPHA+ Kahama), chini ya usimamizi wa Wizara za Afya, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Elimu.

Mkurugenzi Mkazi wa Amref Health Africa Tanzania, anasema shirika hilo litaendelea kuzingatia miongozo inayotolewa na wizara, ili kuhakikisha sera na miongozo ya afya ya kitaifa inazingatiwa.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano yaliyofanyika jijini Dar es Salaam , anasema misaada hiyo itawawezesha wahudumu wa afya ngazi ya jamii, kuongeza upatikanaji wa huduma zenye ubora wa juu, zilizo kamilifu na fungamanishi katika jamii zao kwa kulenga Kifua Kikuu na afya ya uzazi.

"Hii itapunguza sana muda uliotumika na umbali na kurahisisha ubebaji wa sampuli zinazohitaji kupimwa, kwani ubebaji huu utahakikisha kwamba sampuli hizo zinafika katika vituo vya kukusanyia katika muda sahihi na kwa usalama," anasema na kuongezea:

"Jambo hili litakuwa na matokeo chanya kwani litaimarisha programu ya afya ya jamii, itapunguza uendeleaji wa ugonjwa wa Kifua Kikuu na kuongeza utoaji huduma za afya ya uzazi."

### MATARAJIO YA MRADI

Dokta Florence anataja miongoni mwa mambo mengine ya mradi huo kuwa ni kuibua na kufatilia wagojwa wa TB katika ngazi ya jamii katika Mikoa hiyo tisa ya Tanzania Bara na Kaskazini Unguja na Mjini Magharibi hadi kufika mwaka 2025.

Anasema mradi huo pia utashughulikia mahitaji ambayo bado hayajatimizwa ya Uzazi wa Mpango kupitia afua za kijamii katika Mikoa minne ya Katavi, Kigoma, Rukwa na Songwe.

### MALENGO YA AMREF

AMREF imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Afya na TAMISEMI katika kuchangia juhudi za serikali kutekeleza miradi ya kuimarisha huduma za afya na maendeleo ya jamii kupitia sera na miongozo ya kitaifa ya afya na kwamba inatekeleza miradi zaidi ya 19 katika Mikoa mbalimbali hapa nchini.

Vile Vile Amref ina miradi yenye mtazamo wa kitaifa kama vile mpango wa elimu kwa njia ya masafa (e-learning) na wa kuimarisha maabara ambao unatekelezwa katika Mikoa tofauti upande wa Bara na ule wa Zanzibar, anasema Dk Florence.

Anaongeza : "Miradi yetu imegawanyika katika maeneo makuu manne ambayo ni Afya ya uzazi, Watoto Wachanga na Vijana (RMNCAH); Udhibiti na Uzuiaji Magonjwa (DCP) ikijumuisha programu za VVU na UKIMWI, TB, Huduma za Maabara, Fistula ya uzazi na lishe; maji safi, Usafi wa Mazingira na Mwili (WASH) na kujenga uwezo kupitia mafunzo ."

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Dk. Grace Magembe, anasema wizara imejipanga kukabiliana na maradhi hayo nchini na kwamba, baiskeli hizo zitatumiwa na watoa huduma wa Wizara hiyo, kwa lengo la kuwafikia wagonjwa walipo nyumbani, ambao kwa sababu mbalimbali wameshindwa kufika hospitalini

Anasema watumishi hao pia watachukua sampuli za makohozi kupima TB kwa vifaa maalum vilivyotolewa na AMREF, ili kumsaidia mgonjwa kupimwa akiwa nyumbani.

"Kupitia Wizara ya Afya, tunashukuru sana kwa baiskeli hizi na makasha ya kukusanyia sampuli za makohozi ya TB, ambavyo vitatumika katika mikoa inayotekeleza mradi huu nchini," anasema Dk. Magembe.

Ananthy Thambinayagam, Mkurugenzi wa Ofisi ya Afya ya Shirika la Marekani la USAID, anasema kupitia jitihada hizo, serikali ya Marekani itaendelea kuisaidia na kushirikiana na Tanzania, Washirika wa Maendeleo, Azaki, vyama vya kiraia vya mahali na wadau wengine kufanya kazi pamoja kuimarisha mfumo wa afya nchini.





# Vifo Ukimwi vyapungua asilimia 50

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amesema vifo vinavyotokana na Ukimwi vimepungua kwa asilimia 50.

Hatua hiyo imetokana na Tanzania kupiga hatua kwenye udhibiti wa ugonjwa huo na matumizi ya dawa za kufubaza makali ya Virusi Vya Ukimwi(ARV).

Waziri Mhagama alisema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizindua Kamisheni ya Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS).

Alisema vifo vinavyotokana na Ukimwi vimepungua kutoka vifo 64,000 mwaka 2010 hadi kufikia 32,000 kwa mwaka 2020.

Mhagama alibainisha kuwa kiwango cha upimaji afya kwa Watanzania kimeongezeka kutoka asilimia 61 kwa mwaka 2016 hadi asilimia 83 kwa mwaka 2019.

"Matumizi ya ARV kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi (VVU) ambao wanajua hali zao za maambukizi yameongezeka kutoka asilimia 95 kwa mwaka 2016 hadi asilimia 98 hivi sasa. Nakupongeza mwenyekiti kwa kuwa uliongoza kamisheni hiyo," alisema.

"Tunaomba wajumbe tunaoingia kwenye kamisheni tuna kazi ya kufanya kuhakikisha vifo haviongezeki, kiashiria cha vifo kuongezeka ni wale wanaoishi na VVU hawajitokezi kupima maana lengo wajitokeze, wajue hali zao na watumie ARV," aliongeza.

Alisema takwimu hizo zinatoa matumaini makubwa huku akisema kiwango cha maambukizi kwa jamii kimeshuka kutoka asilimia saba kwa mwaka 2003/4 hadi asilimia 4.7 kwa mwaka 2016/17.

"Maambukizi mapya kwa watu wazima yamepungua kutoka 110,000 hadi kufikia 68,000 kwa mwaka 2020, tunaona tunakwenda vizuri," alisema.

Hata hivyo, aliitaka kamisheni hiyo kuimarisha mapambano ya maambukizi mapya ya VVU kwa kundi la vijana ambalo utafiti unaonyesha kuwa zaidi ya theluthi moja ya maambukizi hayo hutokea kwa vijana wenye umri wa miaka 15-28 hasa vijana wa kike.

Alisema licha ya kuwapo na mafanikio mbalimbali kwenye mapambano ya ugonjwa huo lakini kuna haja ya kutokomeza maambukizi hayo.

"Ili kufikia malengo ya kidunia ya mwaka 2030 ya kuhakikisha tunakuwa na ziro Ukimwi kwenye mataifa yetu, kuna haja ya kuimarisha jitihada zetu katika kuzuia maambukizi mapya ya VVU hasa kwa vijana," alisema.

Alisema inawezekana kutokomeza maambukizi hayo kama ilivyofanikiwa kuzuia maambukizi ya VVU kwa mama kwenda kwa mtoto.

"Tumepata mafanikio ya kudhibiti maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto kutoka asilimia 18 hadi 7 tuwapongeze kinamama wajawazito tumeokoa sana watoto maana wangezaliwa na maambukizi, kwa hiyo tunaweza hata kwenye kundi hili la vijana na ni ajenda muhimu sana," alisema.

Aidha, alisisitiza kuimarishwa kwa huduma za upimaji na matumizi ya ARV kwa makundi maalum kwa jamii ikiwamo watu wenye ulemavu.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Watu Wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga, alihimiza ushirikishwaji wa kundi la watu wenye ulemavu katika kamisheni hiyo.

Naye Mwenyekiti wa Kamisheni hiyo, Dk. Hedwiga Swai, aliihakikishia serikali kuwa watatimiza majukumu yao kwa weledi kwa kuzingatia sheria ili TACAIDS ifanye kazi kwa ufanisi.

# TARURA yajipanga ujenzi wa barabara

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKALA wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) jijini Dodoma, umejipanga kujenga barabara kwa kiwango cha lami na kukarabati zilizoharibika wakati wa mvua ili kurahisisha usafiri kwa wananchi.

Meneja wa TARURA Jiji la Dodoma, Mhandisi Goodluck Mbanga, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu hoja mbalimbali kwenye Mabaraza ya Madiwani juu ya mipango ya ujenzi wa barabara.

Alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha barabara zinapitika kwa urahisi ili kuchochea maendeleo kwa wananchi.

Alifafanua kuwa barabara ya Zuzu hadi Kizota ni barabara inayohudumia viwanda na inatarajiwa kupandishwa hadhi na kujengwa kwa kiwango cha lami.

"Uboreshaji wa barabara upo katika mpango wa utekelezaji na serikali imefanya kazi kubwa kuboresha barabara za Dodoma hasa barabara ambazo zina umuhimu wa barabara za kimkakati," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa barabara za pembezoni zitaendelea kuhudumiwa na kufanyiwa marekebisho na zitatengenezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Kuhusu kupunguza msongamano, mhandisi huyo alisema barabara za pembezoni zitafanyiwa marekebisho ili kupunguza msongamano katika barabara kuu huku akibainisha barabara ya Medeli kupitia Kisasa hadi Nzuguni itajengwa kwa kiwango cha lami ili kutumika kama njia mbadala.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Mbori, Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma, wakichota maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kwenye Mto Mbori juzi, huku wengine wakiyakanyagaga wakati wakivuka kitendo ambacho ni hatari kwa afya za watumiaji. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mkataba uzalishaji umeme wa makaa ya mawe watiwa saini

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), yametia saini makubaliano ya ushirikiano wa kuanza kuzalisha umeme wa megawati 200 kwa kutumia madini ya makaa ya mawe Kiwira ili kuongeza nguvu kwenye gridi ya taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dk. Tito Mwinuka, alisema juzi kuwa utekelezaji wa mradi huo utaanza baada ya wataalamu kukamilisha upembuzi yakinifu.

"Mkataba huu ni makubaliano ya awali kati ya TANESCO na STAMICO na baada ya hapa wataalamu wataendelea na utaratibu wa kufanya upembuzi kuhusu mradi huu ambao utakuwa wa kwanza hapa nchini kutumia makaa ya mawe," alisema.

Alisema mradi huo utapunguza gharama za umeme na utaongeza nguvu ya umeme kwenye gridi ya taifa.

Dk. Mwinuka alibainisha kwa sasa kuna vyanzo viwili vya uzalishaji wa umeme nchini ambavyo ni gesi inazalisha kwa asilimia 55 na maji asilimia 36 na kuongeza kuwa a uzalishaji huo wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe kwa mara ya kwanza utakuwa chanzo cha tatu za uzalishaji wa umeme nchini.

Mkurugenzi huyo alisema rasilimali hiyo ya makaa ya mawe ilikaa kwa muda mrefu bila kutumika na utakapoanza utatoa megawati 200 zitakazoingia kwenye gridi ya taifa.

Alifafanua kuwa umeme huo utatoka Kiwira hadi Mbeya na utawanufaisha wananchi waliopo njiani kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kupitisha umeme huo.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji STAMICO, Dk. Venance Mwasse, alisema kuna zaidi ya tani milioni 300 za makaa ya mawe katika eneo hilo la Kiwira.

Dk. Mwasse alisema nguvu hiyo ya umeme itakayozalishwa hapo kwa kutumia madini hayo na inaweza kutumika zaidi ya miaka 2000.

Alisema uzalishaji huo wa umeme kwa kutumia madini hayo utasaidia kuyaongeza thamani kutokana na kukaa muda mrefu bila kutumika.

Kadhalika, alisema uzalishaji wa umeme kwa njia hiyo utakuwa na manufaa makubwa katika taifa kuhusu kutekeleza sera ya viwanda ambavyo vinahitaji umeme wa kutosha.





# Adaiwa kumuua mpenziwe kisha na yeye kutaka kujiua kwa sumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKAZI wa Kata ya Inyala katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mabula Joseph (36), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumuua mpenzi wake, Jema Mela (36), aliyekuwa Mwalimu wa Shule ya Msingi Inyala kwa kumcharanga na mapanga kisha naye kujaribu kujiua kwa sumu.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi saa 1:00 asubuhi kwenye nyumba ya shule alimokuwa anaishi mwalimu huyo.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa kimapenzi kwa madai kuwa kabla ya mtuhumiwa kutekeleza unyama huo, Mela alimwambia kuwa hataki kuendelee na uhusiano jambo ambalo lilimkasirisha na kuamua kumuua.

Kamanda Matei alisema baada ya kumuua mwanamke huyo, mtuhumiwa alijaribu kujiua kwa kunywa sumu aina ya Suraquat, lakini wakati anatapatapa alikolewa na polisi kwa kushirikiana na wananchi na kisha kumpeleka hospitalini ambako anatibiwa katika chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi (ICU) chini ya ulinzi.

"Katika eneo la tukio kulikutwa panga ambalo lilitumika kumuua mwalimu huyo na lilikutwa pia kopo lenye mabaki ya sumu ambayo mtuhumiwa alijaribu kuinywa ili ajiue. Sasa tunamshikilia kwa ajili ya hatua zaidi ikiwamo kufikishwa mahakamani," alisema Kamanda Matei.

Aliwataka wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi na badala yake wanatakiwa kumaliza matatizo yao hasa ya kifamilia kwa kufuata njia sahihi ikiwamo ya kutumia vyombo vya kisheria.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amesema matukio ya wananchi kuuana kwa sababu ya wivu wa kimapenzi yameongezeka katika mkoa wa Mbeya kwa madai kuwa hivi karibuni matukio kama hayo yalitokea katika miji ya Mbalizi na Igurusi wilayani Mbarali.

Aliwaagiza viongozi wa vijiji na kata zote za mkoa kushirikiana kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna sahihi ya kumaliza matatizo ya kifamilia badala ya njia inayotumika sasa hivi ambayo alisema inaleta taswira mbaya.

"Naagiza watendaji wa vijiji na kata, maofisa maendeleo ya jamii na polisi kata katika maeneo yote kutoa elimu kwa wananchi ili waachane na mambo haya ya kuuana kijinga kwa sababu ya wivu wa mapenzi, matukio haya yanaonyesha kuwa hawa watu wanakuwa hawajitambui," alisema Homera.

Aliliagiza Jeshi la Polisi mkoani pia kushiriki kutoa elimu kwa wananchi ili kukomesha matukio hayo ambayo yamekuwa yakigharimu maisha ya watu wasiokuwa na hatia na akasisitiza kuwa hataki kusikia tena mauaji ya kikatili kama hayo.

Alisema yeyote atakayekamatwa akitekeleza matukio hayo anatakiwa kuchukuliwa hatua kali za kisheria ili liwe fundisho kwa watu wengine wenye nia kama hizo.



Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO), Dk. Alexander Kyaruzi (mbele), akiwaongoza wajumbe wa bodi hiyo kukagua maeneo yatakayotumika kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jotoardhi kwenye Ziwa Ngosi, mkoani Mbeya juzi, kazi inayofanywa na Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi nchini (TGDC). **PICHA: NEBART MSOKWA**

# NMB yazindua mikopo riba nafuu

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

BENKI ya NMB imezindua huduma mpya ya mkopo wenye riba nafuu kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wenye kipato cha chini kutekeleza takwa la kisheria la kurasmisha makazi yao ijulikanayo kwa jina la 'NMB Plot Loan'.

Kaimu Afisa Mkuu Ukaguzi wa Ndani wa NMB, Benedicto Baragomwa, aliyasema hayo juzi wilayani hapa wakati wa uzinduzi rasmi wa Programu ya Kitaifa ya Urasimishaji wa Makazi ambayo inatekelezwa kwa ushirikiano kati ya benki hiyo na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Alisema Benki ya NMB itawasaidia wananchi kulipia gharama zote za urasimishaji wa makazi kuanzia upimaji wa viwanja mpaka uandaaji wa hatimiliki na kwamba mwananchi atalipa kidogo kidogo ndani ya miaka miwili.

Alisema riba ya mkopo huo ni asilimia 10 na kwamba mwananchi atapatiwa hatimiliki baada ya kukamilisha urejeshaji wa mkopo wake katika benki hiyo.

"Tumeanzisha huduma hii kwa sababu kuna baadhi ya wananchi wamekuwa wakishindwa kurasmisha makazi yao kutokana na kukosa fedha za kulipia gharama za urasmishaji. Wananchi wakisharasimisha makazi yao na kupatiwa hatimiliki, watakuwa na sifa za kukopesheka katika benki yoyote," alisema Baragomwa.

Alisema mwananchi yeyote ambaye atakopeshwa atafunguliwa akaunti ya NMB bila gharama yoyote na kwamba kuwa fedha hizo zinapitia benki na hata marejesho yatapitia benki.

Akizindua programu hiyo ya urasmishaji wa makazi kitaifa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, aliipongeza NMB kwa kuanzisha huduma hiyo akidai kuwa itasaidia wananchi kupandisha hadhi makazi yao.

Alisema asilimia kubwa ya wananchi wanaishi kwenye makazi holela ambayo yamejengwa bila kufuata sheria, hivyo serikali badala ya kuyabomoa imeamua kuyarasimisha ikishirikiana na NMB, ushirikiano ambao alisema haujawahi kutokea.

Lukuvi alisema kwa mujibu wa sheria kila mwananchi anatakiwa kujenga nyumba kwenye kiwanja kilichopimwa, chenye hatimiliki na lazima apate kibali cha ujenzi kitu ambacho alisema Watanzania wengi hawatekelezi, hivyo kuwa na idadi kubwa ya makazi holela.

"Tulianza kutekeleza urasmishaji huu wa makazi mwaka 2013, lakini mpaka sasa tumefikia asilimia tano pekee nchi nzima. Hii ilikuwa inasababishwa na wananchi wengi kukosa fedha za kugharimia. Sasa hii huduma ya 'NMB Plot Loan' itatusaidia kurasimisha makazi mengi zaidi," alisema Lukuvi.

Alisema awali gharama za urasimishaji wa makazi ilikuwa Sh. 150,000 lakini sasa hivi serikali imepunguza kiwango hicho na kufikia Sh. 130,000 na kwamba kwa sasa gharama hizo zitabebwa na NMB na wananchi watalipa kidogo kidogo.

Likuvi alisisitiza kwamba kwa sasa mtu yeyote ambaye amejenga mjini ni lazima arasimishe makazi yake tofauti na wale wanaoishi maeneo ya vijijini ambao utaratibu utaendelea kuboreshwa.

# Tatizo la maji kuwa historia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kijiji cha Ilota katika Kata ya Mshewe Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanatarajiwa kuondokana na tatizo la muda mrefu la kutembea umbali mrefu kutafuta maji kwenye makorongo.

Hatua hiyo inatokana na serikali kutoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya kuwapelekea maji ya bomba.

Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza aliyasema hayo juzi alipofanya ziara na kuzungumza na wananchi wa kijiji hicho kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye kijiji hicho.

Alisema wananchi hao wanaunganishiwa maji kutoka kwenye Mradi wa Maji wa Shongo ambao unahudumia Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi na Bonde la Songwe na kwamba mradi huo utakamilika hivi karibuni.

Alisema mtaro wa kupeleka maji unachimbwa na vijana wazawa wa kijiji hicho kutoka Mbalizi na kwamba endapo itaonekana wanachelewa kumaliza watachukuliwa vijana kutoka katika maeneo mengine ili waungane nao.

"Kinachochelewesha vijana wetu kuchelewa kufika ni kwa sababu ardhi kwa kipindi hiki ni ngumu, lakini wakikazana tunaweza tukapata maji ndani ya wiki tatu hivyo nawaomba tuongeze ushirikiano kwenye hili jambo," alisema Njeza.

Baadhi ya wanawake wa kijiji hicho walisema katika kijiji hicho hawajawahi kupata maji ya bomba na badala yake wamekuwa wakihangaika kwenda kuchota makorongoni ambako hawana uhakika na usalama wake.

Mmoja wa wananchi hao, Juma Ndamile aliiomba serikali kuwaajiri vijana wa maeneo mengine ili kuharakisha kuchimba mrato huo na wananchi waanze kupata maji haraka.

Alisema maji kwenye kijiji hicho ni tatizo la muda mrefu hasa kipindi cha kiangazi ambacho anadai huwa yanakauka na kuwalazimu wanawake kutumia muda mrefu kwenda kuchota yaliyotwama kwenye makorongo.

Alisema wakati mwingine wamekuwa wakiumwa matumbo bila kujua sababu na kwamba kuna uwezekano chanzo ikawa ni aina ya maji ambayo wanakunywa.

"Tunajua kwamba hii ni ajira kwa vijana wetu, lakini lengo letu tupate maji haraka, kama inawezekana tunaiomba serikali itusaidie hata vijana wa maeneo mengine ili kazi iishe haraka tuanze kunywa maji ya bomba," alisema Njeza.

Naye Oliver Steven alisema wamekuwa wakiamka usiku kwenda kuchota maji hali ambayo imekuwa ikisababisha migogoro kwenye ndoa kutokana na kutoaminiwa na waume zao.

Alisema wanawahi alfajiri lakini wanarudi na maji mchana wakiwa na ndoo moja kila mtu kutokana na maji hayo kupatikana kwa kiwango kidogo.



# Makamu Abdulla ataka ufanisi mazingira ya kazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka watendaji wa serikali kusimamia vyema dhamana walizokabidhiwa ili kuongeza ufanisi katika mazingira ya kazi.

Hemed alitoa agizo hilo jana wakati alipofanya ziara ya kushtukiza katika Kituo cha Damu Salama kilichopo Sebleni, Amani mjini hapa.

Alisema wapo watendaji wazembe wasiopenda kutekeleza majukumu katika sehemu zao za kazi na kusema serikali itachukua hatua kwa lengo la kuimarisha utendaji katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Alisema Kituo cha Damu Salama kina umuhimu mkubwa katika kuokoa maisha ya watu na kuna kila sababu kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia kituo hicho kufanya kazi kwa uadilifu na uaminifu ili kufanikisha lengo lilokusdiwa.

Akikagua maabara maalum ya kuchunguza na kuhifadhia damu, Abdulla alimtaka msimamizi wa maabara hiyo kuwa makini katika kuhakikisha damu hizo zilizochangiwa kwa hiari na wananchi na zinahifadhiwa kwa umakini mkubwa.

Aidha, katika kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizowasilishwa na wafanyakazi, alimtaka Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Abdalla Suleiman, kuzichukua changamoto hizo na kupitia uongozi wa Wizara ya Afya aangalie namna bora ya kuzipatia ufumbuzi.

Akizungumzia changamoto ya gari maalum ya shughuli za damu salama, aliitaka Wizara ya Afya kutoa kipaumbele kwa kulifanyia matengenezo gari hilo ili liendelee kutumiwa na wafanyakazi katika kazi zao za kila siku.

Katika hatua nyingine, Abdulla alisema hakuridhishwa na utaratibu wa kuzihifadhi taka katika kituo hicho huku akimwagiza Mkurugenzi Mkuu kuwasilisha taarifa kamili juu ya kuharibika kwa kifaa maalum cha kuchomea taka ili kuepuka kuzagaa katika maeneo yasiyokuwa rasmi.

Akielezea changamoto zinazowakabili wafanyakazi katika kituo hicho, Fundi Sanifu wa damu salama, Madina Abdalla Khamis, alimweleza Makamu wa Pili wa Rais kuwa, kituo hicho kinakabiliwa na tatizo la uhaba wa vifaa vya kufanyia kazi ikiwamo usafiri, majokofu ya kuhifadhia damu pamoja na mashine ya kufulia.

Akiwa katika Kituo cha Afya cha Mtipura, aliwaagiza wasimamizi wa kituo hicho kuangalia namna bora ya kutoa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia wakati wanaofika vituoni wakizingatia kuchukua tahadhari ya kuwakusanya watu wengi kwa muda mrefu kutokana na maradhi ya Covid-19 na kufanya ukarabati kwa maeneo ambayo hayapo vizuri.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, ACP Awadh Juma Haji, akizungumza na madereva bodaboda (hawapo pichani), wakati wa kikao cha kukumbushana kufuata Sheria za Usalama Barabarani katika Viwanja vya Polisi Madema Visiwani Zanzibar juzi. Kulia ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Khamis Hamza Chilo. **PICHA: WMNN**

# ‘Changamkieni fursa huduma za fedha za masoko’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Yussuf Masauni, amewataka wananchi wa Zanzibar, kuzichangamkia fursa za huduma za fedha za masoko kwa ajili ya kuwainua kiuchumi.

Alisema watakapochangamkia fursa hizo watapiga hatua kubwa ya maendeleo, pia kupunguza malalamiko ya ukosefu wa ajira kwa vijana.

Aliyasema hayo mjini Zanzibar, wakati akifungua ofisi za taasisi ya kifedha ya UTT AMIS, Michenzani Zanzibar.

Alisema huduma za masoko ya fedha lengo lake kubwa kuwawezesha Watanzania kufaidika na kuzitumia fursa za fedha kuwainua kiuchumi na maendeleo.

Alisema kuwapo kwa ofisi za taasisi hiyo ni sehemu ya mikakati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuona kwamba Watanzania wote wanafaidika na fursa za kifedha na kupata maendeleo.

Masauni alisema amefurahishwa na uongozi wa taasisi hiyo kupokea maelekezo ya maagizo aliyowapa ikiwamo kufungua ofisi zake Zanzibar na hivyo kutoa ushirikishwaji mpana wa wananchi kufikisha huduma za kifedha katika pande zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

“Nimefurahishwa na uamuzi wenu wa kufungua ofisi zenu Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano hatua ambayo itasaidia kuwawezesha wananchi wote kufaidika na fursa za huduma za kifedha na kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya kiuchumi na kupambana na umaskini,” alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi ya taasisi hiyo, Juma Muhimbi amesema Taasisi ya UTT AMIS imepiga hatua kubwa na kufanikiwa kufunguwa matawi matano nchini kote ikiwamo Arusha, Mwanza, Mbeya na Zanzibar.

Alisema UTT AMIS imepiga hatua kubwa katika kutoa huduma zinazolenga na kuwawezesha wananchi kiuchumi ikiwamo kuanzisha jumla ya mifuko sita ambayo wananchi wataweka fedha kwa ajili ya kufaidika na fursa za hisa.

“Taasisi ya UTT AMIS inaendelea na utoaji wa huduma zake kwa wananchi ambapo hivi sasa tumefanikiwa kufikia jumla ya mikoa sita ikiwamo Zanzibar,” alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo ya UTT AMIS, Simon Migangala, alisema hadi kufikia Juni 2020, wamefanikiwa kulipa gawio la fedha serikalini jumla ya Sh. bilioni 1.6 hatua ambayo inaonyesha wazi kwamba taasisi hiyo imekuwa ikiendesha shughuli zake kwa mafanikio makubwa.

“Tupo nchini kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kufaidika na fursa za fedha na uwekezaji kiuchumi huku tukipata mafanikio hatua kwa hatua kutokana na ubunifu wa hali ya juu,” alisema.

UTT AMIS ni Taasisi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikiwa chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ambayo lengo lake kubwa kuwawezesha wananchi kiuchumi na kujiwekea akiba na kuwekeza katika masoko ya fedha na mitaji.

## SMZ yafanya mabadiliko sheria kulinda uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya mabadiliko katika Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Namba 14 ya mwaka 2018.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika Ofisi za Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema mabadiliko hayo yamelenga kufungua fursa zaidi za uwekezaji mkakati kwa upande wa Pemba.

Alisema pia mabadiliko hayo yamelenga kuongeza fursa na vivutio vipya kwa wawekezaji wa biashara ya majengo pamoja na wanunuzi wa nyumba zilizoko katika miradi ya uwekezaji kwa Unguja na Pemba.

Alisema mabadiliko hayo yaliyofanyika yamehusisha uongezaji na ufutaji wa baadhi ya vifungu na aya katika jedwali namba tatu na sita pamoja na kuongeza sehemu ya tatu katika jedwali namba sita ya Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar.

“Miongoni mwa vifungu vilivyoongezwa ni pamoja na kuipa hadhi ya uwekezaji mkakati kwa uwekezaji unaoanzia kiwango kisichopungua Dola za Kimarekani milioni 10 katika kisiwa cha Pemba,” alisema Soraga.

Pia alisema mapendekezo hayo yana lengo la kutoa vivutio vya ziada kwa waendelezaji na wanunuzi wa biashara ya kuendeleza nyumba.

Alisema jumla ya vivutio na fursa nane vimeongezwa kwa mwekezaji mkakati aliyewekeza katika biashara ya majengo.

Alisema kwa upande wa waendelezaji wa miradi ya biashara ya majengo ikiwamo maduka makubwa, nyumba ya biashara, vituo vya mikutano vitakuwa na msamaha wa asilimia 100 ya kodi za zuio la ulipaji wa riba.

“Kwa upande wa wanunuzi wa nyumba, vivutio ni pamoja na kupatiwa kibali cha ukaazi kwa mume au mke na watoto wanne waliochini ya miaka 20... kivutio hicho ni kwa mnunuzi wa nyumba yenye thamani isiyopungua Dola za Kimarekani 100,000 kwa miradi ya kimkakati iliyoidhinishwa na mamlaka.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA RUFAA JINAI Na. 72 /2018**

**(Asilia Shauri la Jinai Na.3/2017,Mahakama ya Wilaya ya Rungwe)**

**JAMHURI..........................................................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**ISRAEL ANANGISYE.................................MJIBU RUFAA**

**KWA : ISRAEL ANANGISYE,**

**POPOTE ULIPOTANZANIA.**
**KUITWA SHAURINI**

ELEWA KWAMBA,Ukikosa kufika siku hiyo Unaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya Tarehe 13/08/2021 siku ya Ijumaa Saa3.00 asubuhi bila kukosa,ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.
, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila WEWE kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 13 Mwezi Julai, 2021.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

116404202

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.... 2021**

**In the matter of the Estate of the late ISACK MUSSA CHIWANGA of Mbwanga area within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SARAH MICHAEL CHINYELE AND NOEL HADSON CHIWANGA**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before **18TH Day of August 2021.**
Presented for filling this 05 day of 08 2021.

RESIDENT MAGISTRATE

16404302

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.239/2021**

116404402

Ombi la **RAJABU HOSSENI ALLY** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **HOSSENI RAJABU ALLY**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 13/09/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 10/08/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya wilaya ya MAKOLE**
**Wilaya ya DODOMA**
**MADAI NAMBARI 92/2021**
**MDAI GEOFREY IBRAHIMU**
**MDAIWA ANJELICK MZIRAYI**
**Kwa ANJELICK MZIRAYI**
**MOSHI.**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA PESA TASLIMU TSH 755,000/=**

Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya **JUMANNE Tarehe 24/08/2021 saa 2.30** asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama itadhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo **tarehe 11/08/2021.**

116404602

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Papa Francis atumiwa bahasha yenye risasi

**Vatican City, ITALIA**

BAHASHA iliyo na risasi tatu ndani yatumwa kwa kiongozi wa kiroho wa Wakatoliki Papa Francis.

Bahasha iliyo na risasi tatu ilitumwa kwa kiongozi wa kiroho wa Wakatoliki duniani.

Risasi tatu za milimita tisa na ujumbe juu ya shughuli za kifedha huko Vatican zilipatikana ndani ya bahasha hiyo iliyofika ofisi ya posta karibu na Milan, Italia.

Wafanyakazi wa Posta ambao walipata bahasha iliyotumwa kwa Papa Francis mara moja waliwaarifu polisi.

Maofisa wa polisi walichukuwa bahasha hiyo na kuanzisha uchunguzi juu ya tukio hilo.

Ilitangazwa kuwa bahasha ilitumwa kutoka Ufaransa na anuani "Papa, Jiji la Vatican, Mraba wa Mtakatifu Petro, Roma," ziliandikwa juu yake.

Hadi kufikia sasa bado hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na Vatican.

**TRT**

# Moto waua wanajeshi 25 waokoaji

**Algiers, ALGERIA**

WATU wapatao 42 wamefariki kutokana na moto uliotokea katika maeneo zaidi ya 100 ya porini, Algeria.

Moto mkubwa zaidi umetokea katika maeneo ya milima katika mkoa wa Kabylie, wanajeshi 25 wamefariki wakati wakipambana kuzima moto huo.

Rais wa Algeria, Abdelmajid Tebboune, ametuma salamu za rambirambi kwa familia za wahanga, alisema wanajeshi wameweza kuwaokoa watu zaidi ya 100 kutoka kwenye moto.

Waziri wa Mambo ya Ndani anawashuku kuwa wachomaji misitu wanahusika na janga hilo la moto.

Matukio ya moto katika eneo la pori katika mataifa ya ukanda wa Mediterranea yamezidi kutokana na joto kuongezeka na kiwango cha ukame kuongezeka.

Mji Mkuu wa Tunisia, Tunis, umeshuhudia kiwango cha juu zaidi cha joto cha nyuzi joto 48C Jumanne.

.

**BBC**

# 24 familia moja wafa kwa kula sumu Nigeria

**Lagos, NIGERIA**

WATU 24 wa familia moja wamefariki dunia kwa kula sumu walidhani ni chumvi kumbe ilikuwa mbolea.

Tukio hilo limetokea Kaskazini magharibi mwa Nigeria katika Kijiji cha Danzanke, Jimbo la Sokoto.

Kamishna wa Afya wa Jimbo la Ali Inname aliwaambia waandishi wa habari kwamba familia hiyo, ilitumia kimakosa kemikali ya mbolea ambayo ilionekana kama chumvi wakati wa kuandaa chakula Jumatatu.

Alisema wafanyakazi wa matibabu walijaribu kuokoa maisha ya waathiriwa bila mafanikio.

Hata hivyo watu wawili wa familia ambao walionja tu chakula hicho sasa wanapata matibabu hospitalini.

Kufuatia tukio hilo, maofisa wameshauri tena watu kuweka vitu vyenye sumu mbali na maghala yao ya chakula kwa sababu za usalama.

Matukio kama hayo yanayohusu familia kufa kwa kula sumu yametokea huko Nigeria, idadi ya waliokufa katika tukio hili la hivi karibuni ni kubwa sana.

***BBC***



Magari yakiwamo ya abiria yakiwa yameharibiwa na maporomoko ya udongo, na kuua watu wawili na makumi kujeruhiwa Kaskazini mwa India, Jimbo la Himachal Pradesh, jana. **PICHA: BBC**

# Abiy ataka raia kupambana na waasi

**Addis Ababa, ETHIOPIA**

SERIKALI ya Ethiopia imewataka raia wenye uwezo kujiunga na jeshi kupambana na vikosi vya Tigray.

Abiy amewataka Waethiopia wajiunge na majeshi ya ulinzi, vikosi maalumu na kuonyesha uzalendo wao.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, ametoa kauli siku ya juzi kuwahimiza raia wa nchi hiyo kujiunga na jeshi kuwachakaza wapiganaji wa vikosi vya Tigray wanaoendeleza mapambano.

Wito huo umewashtua Watigray hata wale wanaoishi nje ya nchi, huku Abiy akiwataka Waethiopia wawe macho na masikio ya nchi ili kuwafuatilia na kuwafichua majasusi na mawakala wa vikosi vya Tigray.

Watu walioshuhudia na mawakili walisema maelfu wa Watigray tayari wamekamatwa na wanazuiliwa wakati wa mzozo kutokana na utambulisho wao pekee.

Teklehaymanot G. Weldenmichel, ambaye familia yake imenasa Tigray, alisema aina ya vita anavyoitisha Waziri Mkuu viko katika ngazi nyingine tofauti kabisa wito wake ukiwa na maana ya kusafisha kila mtu.

Wito wa kujiunga na vita kwa sasa si wa lazima, lakini kwa sababu watu wamezuiwa kuyafikia maeneo mengi ya Ethiopia, ni vigumu kufahamu aina ya shinikizo linalotumika.

Kauli ya Abiy imetolewa wakati Shirika la Umoja wa Mataifa linalowahudumia Wakimbizi (UNHCR), likisema limefanikiwa kuzifikia kambi za wakimbizi katika eneo la Tigray.

Akizungumza mjini Geneva, msemaji wa UNHCR, Boris Cheshirkov, alisema, "UNHCR na washirika wake wamefanikiwa kuingia kambi za wakimbizi wa Eritrea za Mai Aini na Adi Harush katika eneo la Tigray.

"Hata hivyo hali ya usalama bado inakwamisha kuyafikia maeneo mengi na wakimbizi wanaendelea kukabiliwa na hali ngumu.

"Huduma za msingi kama vile matibabu na huduma za afya bado hazipatikani na majisafi ya kunywa yanakaribia kuisha."

***VOA***

# GREALISH

## ASEMA ALILIA KAMA MESSI



**LONDON, England**

JACK Grealish amesema kuondoka kwake Aston Villa alijihisi uchungu na kutoa machozi kama ilivyokuwa kwa Lionel Messi, wakati akitangaza kuondoka Barcelona.

Grealish aliondoka klabu yake ya utotoni ya Aston Villa na kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City.

Grealish alijiunga na City kwa ada iliyoweka rekodi katika historia ya soka la Uingereza ya pauni milioni 100.

Uhamisho wa Grealish ulifanyika siku moja na Barcelona wakati wakitangaza kuwa hataweza kumwongezea Messi mkataba kutokana na ukubwa na sheria za fedha za LaLiga.

Messi mwenyewe alithibitisha kuondoka hapo siku iliyofuata na kutangaza kwamba, anakwenda Paris Saint-Germain na juzi Jumanne alisajiliwa rasmi, kwa miaka miwili.

Grealish alikuwa Villa tangu akiwa na umri wa miaka sita na aliwaambia waandishi wa habari kwamba, wakati wa kuaga alijisikia huzuni sana kama ilivyokuwa kwa Messi.

"Kila mmoja ameona namna Messi alivyojisikia uchungu kwenye mkutano wake wa mwisho," alisema Grealish.

"Na mimi nilijihisi vile vile wakati naaga Aston Villa.

"Kabla sijaondoka nilizungumza na timu, benchi la ufundi na wachezaji na nililia mwenyewe."

## UMTITI AWEKA SHARTI KUONDOKA BARCA



**BARCELONA, Hispania**

SAMUEL Umtiti alikuwa anatajwa kwenye mpango wa Barcelona kuwauza wachezaji, ili kupunguza gharama za mishahara klabuni hapo.

Barcelona wametumia muda mwingi kutafuta ufumbuzi wa kupunguza gharama za mishahara, ili waweze kumsajili Lionel Messi, ambaye ameondoka klabuni hapo, bila kukiuka taratibu za mishahara za LaLiga.

Baada ya Umtiti kuzomewa na mashabiki kwenye mechi ya Barcelona, dhidi ya Juventus ya Kombe la Joan Gamper Trophy Jumapili, Umtiti amerejea msimamo wake wa sharti ambalo linaweza kumwondoa yeye klabuni hapo.

Baadhi ya mashabiki wanaamini nyota huyo ana mchango wake kwenye sakata la Messi kuondoka Barca, na walikuwa wakimzomea kwenye mechi hiyo, kwa sababu ya hisia hizo.

Kwa mujibu wa Mundo Deportivo, Umtiti yupo tayari kuondoka Barcelona, wakati wakiendelea kuweka sawa vitabu vyao vya fedha.

Hata hivyo, ili nyota huyu aweze kuondoka klabuni hapo, anadai ni lazima kuwe na ofa iliyowasilishwa na klabu yenye ushindani na inayopambania mataji makubwa.

# PSG BADO WAMPIGIA HESABU POGBA

**PARIS, Ufaransa**

PARIS Saint-Germain bado wanamtazama kwa ukaribu nyota wa Manchester United, Paul Pogba kwa ajili ya kukamilisha usajili wake.

Kwa mujibu wa Sky Sports imeeleza iliripoti Julai kwamba timu hiyo ya Ufaransa inahitaji kumpata nyota huyo anacheza ndani Ligi Kuu England.

PSG inahitaji kumsajili Pogba msimu huu kabla ya mkataba wake kumalizika ndani ya kikosi cha United.

Licha ya kwamba PSG imemtambulisha Lionel Messi kuwa ni mchezaji wao bado wana nafasi ya kumpa dili Pogba ikiwa watamhitaji kwa fedha kamili ama kwa mkopo.

Pogba mwenyewe ameonyesha nia ya kutotaka kuendelea kucheza pale United, kwani hadi sasa hajasaini mkataba mpya.

Mkataba wa sasa wa Pogba unamalizika majira ya kipindi cha joto kinachokuja na hivyo kuna uwezekano mkubwa akaondoka kama mchezaji huru.



HABARI MICHEZO



# VARANE
## HATUA MOJA KUTUA UNITED

**MANCHESTER, England**

RAPHAEL Varane jana alifanyiwa vipimo vya kwanza vya afya yake ikiwa ni sehemu ya kukamilisha mpango wake wa kujiunga na Manchester United akitokea Real Madrid.

United, ina matumaini ya kukamilisha usajili wake ndani ya saa 24 hadi 28 zijazo baada ya makubaliano rasmi na Real Madrid, kukamilika mwezi uliopita na ada yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 41.

Varane mwenye umri wa miaka 28, aliwasili Manchester United wiki iliyopita na kukaa karantini kwa siku kadhaa kabla ya kuanza taratibu hizo za vipimo.

Mlinzi huyo wa kati mshindi wa Kombe la Dunia mwaka 2018, atakuwa na usajili wa tatu wa United kipindi hiki cha majira ya joto baada ya ujio wa winga, Jadon Sancho kutoka Borussia Dortmund kwa pauni milioni 73 na Tom Heaton aliyetua, kwa uhamisho huru.

Varane, ambaye mkataba wake Real Madrid ulikuwa unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja, amecheza jumla ya mechi 360, kwa miamba hao wa Hispania kwa kipindi cha mwongo mmoja aliokaa hapo, akishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na LaLiga mara tatu.

United wanataka kukamilisha usajili wa Varane haraka, ili aweze kuanza mazoezi kuelekea mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu England, dhidi ya Leeds United pale Old Trafford, Jumamosi.

# TUCHEL AFUNGUKA
## KILICHOMKWAZA ABRAHAM

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel amesema mshambuliaji, Tammy Abraham ana 'sababu' ya kutokuwa na furaha klabuni hapo baada ya kukosa nafasi ya kucheza mara wa mara msimu uliopita.



Sky Italy imeripoti kwamba, Roma imefikia makubaliano ya pauni milioni 34 kumsajili Abraham, dili ambalo linaweza kutangazwa wakati wowote.

Abraham alimaliza msimu uliopita akifunga mabao 12, lakini alicheza mechi saba tu baada ya Tuchel kuchukua mikoba ya Frank Lampard Januari, huku Romelu Lukaku akikaribia kutua Chelsea, akitoka Inter Milan.

Tuchel amesema Abraham, ambaye alicheza muda wote kwenye maandalizi ya msimu mpya, anaweza kuwa na nafasi ya kucheza msimu huu kama akibaki.

"Siwezi kuzungumza lolote kuhusu ofa ya Roma - namna gani ni kweli au siyo kweli hilo sio jambo langu," alisema Tuchel.

"Tammy kwa sasa yupo na kikosi chetu na amefanya maandalizi ya kutosha wakati wa kijufua kwa msimu mpya.

"Kwa uhakika kabisa hakuwa na furaha msimu uliopita na sababu kubwa ni kwamba hakupata nafasi ya kucheza na pengine hilo halikuwa kosa langu."

# AGUERO NJE YA
## DIMBA HADI NOVEMBA

**BARCELONA, Hispania**

SERGIO Aguero atakosa michezo kadhaa mwanzoni mwa msimu huu wa 2021/22 baada ya kuumia siku ya Jumapili wakati wa mazoezi.



Fowadi huyo wa Argentina aliumia katika kipindi cha mazoezi Jumapili, na sasa anakabiliwa na kati ya miezi miwili au mitatu nje ya dimba.

Barcelona imetangaza mshindi huyo wa Copa America amepata tatizo kwenye kifundo cha mguu wa kulia, na RACI sasa wameripoti kwamba, baada ya vipimo zaidi, anaweza kuwa nje ya uwanja hadi Novemba.

"Utabiri wa mapema ni kwamba jeraha lilikuwa baya, kwani Aguero hakuhudhuria mkutano wa waandishi wa habari wa Lionel Messi kuaga, wala hakuwepo kwenye mchezo wa Kombe la Joan Gamper, dhidi ya Juventus. Kocha wa Barcelona, Ronald Koeman ilibidi azungumze juu ya hali ya Aguero jana usiku, akikiri kusikitishwa kwake na hali hiyo.

"Inasikitisha kwamba ameumia," Koeman alisema. "Lazima tumngoje apone, lakini ni hatua ya kurudi nyuma kwa sababu alikuwa akifanya mazoezi vizuri. "Ana mengi ya kutoa."

Koeman tayari alikuwa na majeruhi Ansu Fati na Ousmane Dembele, huku Philippe Coutinho akiwa amerudi, lakini alikuwa nje ya mchezo, dhidi ya Juventus pia.

## HABARI MICHEZO




# MESSI AITENGENEZEA PSG HISTORIA MPYA

Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo aeleza namna ambavyo wamefurahia ujio wa nyota...

**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi ataisaidia Paris Saint-Germain kutengeneza historia, kwa mujibu wa Mwenyekiti na Ofisa Mtendaji wa klabu hiyo, Nasser Al-Khelaifi.

PSG walifanikisha kupata saini ya Messi baada ya fowadi huyo kushindwa kuendelea na mkataba wa kuendelea kuichezea Barcelona, ambayo imebanwa na sheria za kifedha na kanuzi za LaLiga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 amehamia hapo Parc des Princes baada ya kufunga mabao 672 katika mechi 778 kwa klabu yake hiyo ya zamani na PSG ndio walifanikiwa kuipata saini yake.

Baada ya Messi kuwasili Jumanne, Al-Khelaifi alisema: "Nina furaha kwamba Lionel Messi amechagua kujiunga na Paris Saint-Germain na tunajisikia fahari juu yake na familia yake kwa ujio wao hapa Paris.

"Hajaficha nia yake ya kutaka kuendelea kucheza katika daraja la juu na kushinda mataji na uzuri klabu yetu pia ina nia kama hiyo.

"Kuongezeka kwa Messi kwenye kikosi chetu cha duniani ni mipango mizuri kwetu katika harakati za kupata mafanikio.

"Ikiwa inaongoza na makocha wetu wakubwa pamoja na benchi lote la ufundi, nasubiria kuona namba timu itakavyotengeneza historia kwa pamoja kwa mashabiki wetu na dunia nzima."

Messi amejiunga na mchezaji mwenzake wa zamani, Neymar na sasa watatengeneza safu ya ushambuliaji ya wakali watatu pamoja na Kylian Mbappe.

Kabla ya hapo PSG pia iliwasajili, Sergio Ramos, Gianluigi Donnarumma, Georginio Wijnaldum pamoja na Achraf Hakimi ili kuimarisha kikosi hicho cha kocha, Mauricio Pochettino.

Messi amesaini mkataba wa miaka miwili wenye kipengele cha kuongeza mwaka mmoja zaidi.

## KWA UFUPI

### MESSI KUONDOA 10 PSG

KLABU ya Paris St-Germain italazimika kuuza hadi wachezaji 10 wa kikosi cha kwanza ili kusawazisha mahesabu yao baada ya kumsajili, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34. Kiungo wa Senegal, Idrissa Gueye (31), kiungo wa Hispania, Ander Herrera (31) na mshambuliaji wa zamani wa Argentina, Mauro Icardi (28) ni miongoni mwa wale ambao wanaweza kuuzwa. ***(Sport)***

### EDERSON, CITY KITAELEWEKA

KLABU ya Manchester City inapanga kufungua mazungumzo mapya na kipa wa Brazil, Ederson mwenye umri wa miaka 27 na kiungo wa England, Phil Foden (21), juu ya mkataba mpya pale Etihad. ***(Mail)***

### UNITED: MARTIAL HAUZWI

MANCHESTER United hawana nia ya kumuuza Anthony Martial msimu huu wa kipindi cha majira ya joto baada ya mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 25 kuhusishwa na uwezekano wa kuhamia Inter Milan. ***(Telegraph)***

### SPURS WAMTAKA MARTINEZ

KLABU ya Tottenham Hotspur bado wanaendelea na mazungumzo ya kumsaini Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 23, licha ya ripoti zinazoonyesha kuwa Inter Milan hawataki kumuuza mshambuliaji huyo wa Argentina. ***(Football Insider)***

### ZAKARIA AGOMBEWA EPL

ARSENAL, Tottenham Hotspur na Everton wana nia ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa Uswisi, Denis Zakaria mwenye umri wa miaka 24, kutoka Borussia Monchengladbach.***(Bild)***

### SHAQIRI HAKIELEWEKI

LIVERPOOL na Lyon wametofautiana sana katika thamani ya Xherdan Shaqiri, na wekundu hao wanataka angalau pauni milioni 12 kwa fowadi huyo wa Uswizi mwenye umri wa miaka 29. ***(Liverpool Echo)***

### BUTA ANUKIA EVERTON

EVERTON wamepanga kutoa ofa ya pauni milioni tatu kwa beki wa kulia wa Antwerp na Ureno, Aurelio Buta mwenye umri wa miaka 24, ambaye ameivutia Celtic. ***(Sun)***

### HOLDING KUBAKIA

ARSENAL wanataka kusalia na mlinzi wa England mwenye umri wa miaka 25, Rob Holding klabuni hapo licha kuzivutia klabu za Newcastle na Leicester. ***(Football.London)***

### RICHARLISON KAMILI

FOWADI wa Everton, Richarlison mwenye umri wa miaka 24, anaweza kucheza kwenye mchezo wa ufunguzi wa msimu Jumamosi dhidi ya Southampton licha ya kutokuwa na mapumziko ya kiangazi baada ya kuiwakilisha Brazil kwenye Copa America na Olimpiki huko Tokyo. ***(Liverpool Echo)***

### CHELSEA NA ZOUMA

CHELSEA wamesimama kidete juu ya thamani ya mlinzi wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26, Kurt Zouma, ambaye amekuwa akiivutia West Ham. Thamani ya nyota huyo ni pauni milioni 25. ***(90 Min)***

### KOUNDE NJIA MOJA

MKURUGENZI wa soka wa Sevilla, Monchi anasubiri Chelsea wampigie simu ili aweze kushinikiza uhamisho wa mlinzi wa Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22 kwa ajili ya kuhamia Stamford Bridge.***(Express)***

## KAGERA SUGAR YAGEUKIA VIJANA

**Na Lilian Lugakingira,BUKOBA**

UONGOZI wa Kagera Sugar umeanza zoezi la kusaka wachezaji chipukizi wenye vipaji kutoka sehemu mbalimbali nchini, kwa ajili ya kuunda kikosi cha timu ya vijana ya umri chini ya miaka 20.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza alisema wachezaji wanaowahitaji ni wa kuanzia umri wa miaka 16, lakini ametoa kipaumbele kwa yosso wanaotoka katika mkoa wa Kagera, ili kuondoa malalamiko ya muda mrefu ya kutowahusisha wenyeji.

"Yamekuwapo malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wa Kagera kuwa Kagera Sugar hatuchukui vijana wenye vipaji vya kucheza mpira kutoka katika mkoa huu, sasa tumeamua kuondoa malalamiko hayo, ili kutoa fursa kwa vijana wenye uwezo kunufaika," alisema Baraza.

Kocha huyo alisema kupitia utaratibu huo wana mpango wa kuteua wachezaji 30 na baada ya hapo watatafuta wachezaji wengine wachache kutoka katika Mikoa mingine halafu watafanya mchujo na hatimaye kubakia na nyota 25, watakaosajiliwa rasmi.

Baraza alitumia fursa hiyo kuwataka vijana kujiamini na kuonyesha uvumilivu na wale watakaokosa nafasi hiyo wasikate tamaa huku wataobahatika kupata nafasi hiyo wacheze mpira inavyopaswa na kwa nidhamu.

Yosso Sued Abdallah kutoka Wilaya ya Bukoba Mjini, alisema Kagera Sugar hawatajutia kwa uamuzi huo maana Mkoa huo una vijana wengi.

"Kama Kagera Sugar wataamua kuchukua vijana wa Mkoa huu watayaona matunda yake, ni kweli tulikuwa tunalalamika kuona timu nzima inayowakilisha Mkoa wetu ina mchezaji mmoja tu anayetoka hapa Kagera, hii ilikuwa haiingii akilini" Abdallah alisema.

# UNILEVER YAJITOSA MBIO ZA WATOTO ROCK CITY

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Unilever Tanzania imekabidhi hundi yenye thamani Sh. milioni 20, kwa waandaaji wa mbio za Rock City Marathon, kwa ajili ya udhamini wa mbio za kilomita 2.5, ambazo ni maalumu kwa watoto zitakazofanyika Oktoba 24, mwaka huu jijini Mwanza.

Hatua hiyo inatajwa kuwa ni mwendelezo wa mkakati wa kampuni hiyo katika kushirikiana na jamii na serikali kwa ujumla katika kuhamasisha, kuibua vipaji, kujenga afya pamoja na kukuza sekta ya michezo nchini. Wakizungumza kwenye hafla fupi ya makabidhiano hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Unilever Tanzania, David Minja pamoja na Mratibu wa mbio hizo, Kasara Naftal walisema ushirikiano huo mpya ni ishara nzuri kwa mustakabari wa mchezo huo, sambamba na ukuaji wa sekta ya utalii katika Kanda ya Ziwa.

"Tumeamua kudhamini tukio hili kwa sababu linawaleta pamoja watu kutoka nyanja mbalimbali katika maisha wakiwemo watoto ambao ni miongoni mwa wadau wetu wakubwa," alisema Minja na kubainisha mbio hizo zitafahamika kama 'Unilever Rock City Junior Challenge.'




Mratibu wa mbio za Rock City, Kasara Naftal (kushoto) akipokea mfano wa hundi yenye thamani ya Sh.milioni 20 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Unilever Tanzania, David Minja (kulia) kwa ajili ya udhamini wa mbio za kilomita 2.5 ambazo ni maalum kwa watoto. Katikati ni Meneja Masoko wa Kampuni ya Unilever Tanzania, Lilian Kibasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Minja alisema 'Unilever Rock City Junior Challenge' inalenga kutoa fursa kwa watoto ambao ni miongoni mwa watumiaji wakubwa wa bidhaa zinazozalishwa na kampuni hiyo, ikiwamo sabuni ya OMO, Sunlight na mafuta ya kujipaka ya Vaseline ambao wataibuka washindi kwenye mbio hizo watajipatia zawadi mbalimbali ikiwamo vifurushi maalum vyenye bidhaa hizo.

"Kwa kuwa bidhaa zetu zinahusisha zaidi matumizi ya kifamilia nitoe wito kwa wazazi na wanafamilia kwa ujumla, wajitokeze kwa wingi huku wakihamasisha watoto, pia washiriki kwenye mbio hizi, ili kuongeza ushindani. Unilever tunawahakikishia kwamba zawadi kwa watoto zitakuwa ni nyingi na za kutosha," Minja alisema.

Kwa upande wake, Naftal alishukuru kampuni ya Unilever kwa kuona umuhimu wa kushirikiana nao katika kuboresha mbio hizo, alisema mbio hizo ni moja ya kivutio kikubwa miongoni mwa matukio yanayotarajiwa kupamba mbio hizi.

Naftal alisema pia, itahusisha utafutaji wa vipaji vya riadha kutoka katika baadhi ya Shule za Msingi za jijini Mwanza kwa wanafunzi wenye umri wa kuanzia miaka mitano hadi 10, ambapo washindi pamoja na kujipatia zawadi mbalimbali kutoka Unilever, pia watapata tiketi zitakazowawezesha kuchuana kwenye kilele cha mbio hizo.

"Tangu kuanzishwa kwa mbio hizi, huu ukiwa ni msimu wa 12 sasa tumekuwa tukihusisha ushiriki wa watoto kwa namna mbalimbali. Ila mwaka huu tunaamini mbio za watoto zinakwenda kutikisa vichwa vya habari," alisema mratibu huyo.

Aliongeza wanatarajia kuona ushindani zaidi katika mbio hizo sasa na wanaamini lengo lao la kuibua vipaji vipya vya riadha linakwenda kutimia.

"Asanteni sana Unilever kwa kuwekeza kwa watoto, tunaamini ndoto na malengo yetu yanaelekea kutimia,"Naftali alishukuru.

Alisema maandalizi ya mbio hizo zinazotarajiwa kuhusisha washiriki zaidi ya 3,000 wakiwamo wanariadha maarufu wa ndani na nje ya nchi yanaendelea vyema, lakini akitoa wito kwa wadau wote kuendelea kujisajili kupitia njia ya simu na tovuti ya mbio hizo.




Wafanyakazi wa benki ya Exim wa Tawi la Mtwara wakiwa kwenye picha ya pamoja na uongozi na wanafunzi wa Shule ya awali na Msingi ya St. Michael ya mkoani humo mara baada ya kukabidhi vifaa vya michezo kwa uongozi wa shule hiyo, katika kuunga mkono jitihada za serikali za kurudisha michezo mashuleni. Benki hiyo imeshirikiana na mradi wa jamii unaojulikana kama Exim Cares. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaikaribisha Betway Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kimataifa ya michezo ya kubashiri, imeingia rasmi katika soko la Tanzania ikijipanga kutoa huduma bora na rahisi kwa wapenzi wa michezo ya kubashiri hapa nchini.

Wakati kampuni inaanzishwa mwaka 2006, lengo la Betway lilikuwa ni kuleta ushindani katika tasnia ya michezo ya kubashiri.

Hii imetuwezesha kuingia kwenye soko la Tanzania tukiwa na michezo mingi, yenye masoko tofauti ya kubashiri, mfumo wetu wa kubashiri Live na eSports ni wa kisasa zaidi.

Tunajivunia kufanya kazi katika nchi ambazo, sekta ya michezo ya kutabiri imeratibiwa, kwa sasa tuna leseni za kufanya kazi katika nchi 12 ikiwa ni pamoja na Kenya, Ghana, Afrika Kusini, Uganda, Zambia, Msumbiji na Nigeria. Kwa niaba ya serikali ya Tanzania, Mkurugenzi wa Idara ya Michezo kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Addo Komba ameikaribisha Betway Tanzania na kuwahakikishia ushirikiano kutoka serikalini na kwa wadau wengine wa michezo.

"Ninafurahi kupewa heshima kuwa mgeni rasmi katika hafla hii muhimu sana ya kuikaribisha Betway nchini Tanzania. Serikali inafurahi kuona wawekezaji wapya kama Betway wanaingia Tanzania, kwa nia ya kuunga mkono juhudi za maendeleo katika michezo. Betway ni kampuni kubwa ya michezo ya kubashiri kwa hivyo uamuzi wao wa kuja Tanzania ni ishara nzuri kwetu kwamba tunapiga hatua na wako tayari kutusukuma zaidi," alisema Komba.

Mbali na kutoa burudani ya kusisimua uwanjani, pia tuna mipango kadhaa ya kusaidia jamii nje ya uwanja. Ni kwa mapenzi yetu ya michezo na nia ya maendeleo ya michezo, tunauwezo wa kutoa msaada kwa jamii katika michezo yenye uhitaji.

Meneja Uendeshaji wa Betway Tanzania, Jimmy Masaoe alisema kwamba;

"Ni wakati mzuri katika sekta ya michezo ya kubashiri na tunaamini kwa uzinduzi wa bidhaa hii yenye ubora wa kimataifa kwenye soko, tunauwezo wa kuleta msisimko kwa wanaobashiri na mashabiki, wakati bado tunarudisha kwa jamii kupitia miradi mbali mbali ya michezo."

Kama kampuni ya michezo ya kubashiri, ni jukumu letu kuhakikisha tunaweka mazingira rafiki, kwa ajili ya kubashiri kistaarabu.

# Michezo

Alhamisi Agosti 12, 2021

Nipashe




MESSI AITENGENEZEA PSG HISTORIA MPYA HABARI UK 22




Wachezaji wa Simba ya jijini Dar es Salaam wakiwa wametua nchini Morocco ambapo timu yao inatarajia kuweka kambi maalumu kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki. **PICHA: SIMBA SC**

## YANGA, DJUMA KAMILI MOROCCO

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Yanga imethibitisha rasmi kumsajili beki wa AS Vita, Djuma Shaaban, na atakuwa sehemu ya nyota wa timu hiyo watakaokwenda Morocco kuweka kambi ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2021/22 na mashindano ya kimataifa.

Yanga inatarajia kuelekea Morocco Jumapili lakini ikimtangaza golikipa, Erick Johora Mtanzania aliyekuwa akiichezea klabu ya Agle Noir ya Burundi kuwa sasa ni mali yao.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema Djuma ni mchezaji wao na anakanusha propaganda za kuonyesha hawajamsajili mchezaji huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

"Naona propaganda nyingi zinaendelea. Huyu ndiye mchezaji wa kwanza sisi kumsajili. Labda tu wengi wanaona si kweli kwa sababu hatujamtambulisha. Tumeshindwa kufanya hivyo kwa sababu hajafika Dar es Salaam. Ni mchezaji ambaye atafika nchini ifikapo terehe 14 (Jumamosi) na ataungana na kikosi tayari kwa safari ya kwenda Morocco," alisema Bumbuli.

Kiongozi huyo alisema baada ya kuondoka kwa nyota wao, Tuisila Kisinda sasa nafasi za wachezaji wa kigeni zimebaki mbili, na wachezaji watakaochukua nafasi hizo watatangazwa wakati wowote.

Aliongeza kikosi chao kinatarajia kuweka kambi ya siku 10 huko Morocco na msafara wao utakuwa na watu 44. Ofisa Habari huyo pia aliongeza kilele cha Wiki ya Mwananchi itakuwa ni Agosti 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Naye Mwenyekiti wa Yanga, Mshindo Msolla, alisema mchakato wa usajili wa timu yao unakwenda vizuri na anaamini utawapa matokeo chanya.

"Tuliahidi kusajili wachezaji ambao wataleta ushindani ndani ya timu yetu kwa kuwa mikakati tuliyonayo kwa sasa ni kuchukua ubingwa kwa msimu ujao pamoja na kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa," Msolla alisema.

# Gomes aanza mkwara Simba

## Aahidi kikosi chake kitafanya makubwa zaidi katika msimu ujao...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha kwanza cha Simba kikiwa kimewasili nchini Morocco kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki, Kocha Mkuu, Didier Gomes amesema wana matumaini ya kufanya vizuri zaidi ukilinganisha na msimu uliomalizika.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kutua Morocco, Gomes alisema anatarajia kikosi chake kitakuwa bora na imara zaidi kuliko msimu uliopita kwa sababu wachezaji wake walipata nafasi ya kujifunza mbinu na mikakati mbalimbali.

Gomes alisema wataanza msimu mpya kwa utulivu na umakini, lakini wataziheshimu timu zote watakazokutana nazo katika michuano yote watakayoshiriki ndani na nje ya Tanzania.

"Tuna furaha sana kuanza msimu mpya. Malengo yetu kwanza kabisa ni kulinda rekodi yetu ya msimu uliopita katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu Tanzania Bara. Tunataka kufanya kama tulivyofanya msimu uliopita. Ila tunaweza kuwa bora zaidi msimu huu kuliko uliopita. Kwa sababu si tu kwamba tunataka kufikia malengo, lakini kuivuka ikiwezekana," alisema Gomes.

Kocha huyo aliongeza kila mchezaji wa Simba atatakiwa kucheza kwa kiwango cha juu na uongozi utaendelea kuongeza nguvu katika maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa.

"Ni msimu ambao tunahitaji kufanya kazi kubwa ili kutimiza malengo, tunajua wengi watatuangalia sisi (Simba), kwa sababu ya kile tulichokifanya msimu uliomalizika, ni juhudi tu ndio zitatupa mafanikio," alisema kocha huyo aliyeiwezesha Simba kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.

Naye beki wa timu hiyo, Erasto Nyoni alisema kambi hiyo itawasaidia kupata utulivu na kushika vyema mafunzo watakayopewa na makocha wao kwa ajili ya kufanya vizuri katika mashindano yote watakayochuana katika msimu ujao.

"Tumemaliza mapumziko yetu ya muda mfupi, na sasa tumerejea tena kwa ajili ya msimu mpya. Wanachama na mashabiki wa Simba tunaomba watuombee ili tumalize vyema, turejee nyumbani salama na tufanye vizuri tena katika msimu ujao." Alisema mchezaji huyo mwenye uwezo wa kucheza nafasi zote za nyuma, pamoja na kiungo mkabaji.

Kikosi hicho cha Simba kinatarajia kucheza mechi za kirafiki kabla ya kurejea nyumbani kwa ajili ya kushiriki katika tamasha la utambulisho la Simba Day litakalofanyika Agosti 28, mwaka huu.

Simba na Yanga zitafungua msimu wa 2021/22 kwa kucheza mechi ya Ngao ya Jamii itakayofanyika Septemba 25, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042